

DHIMA YA UFUTUHI KATIKA RIWAYA ZA SHAABAN ROBERT

FORTUNATA MOSES KABEJA

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SHARTI LA KUPATIWA
SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI FASIHI) YA CHUO KIKUU**

HURIA CHA TANZANIA

2013

UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI

Aliyetia saina hapa chini alithibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa “*Dhima ya Ufutuhi Katika Riwaya za Shaabani Robert*”. Kwa ajili ya kusahihishwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ili kukamilisha mahitaji ya Shahada ya Uzamili wa Kiswahili (Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Prof. Dkt. Sheikh T.S.Y.M.Sengo

(Msimamizi)

Tarehe

HAKIMILIKI

Tasnifu hii au sehemu yake yoyote hairuhusiwi kukaririwa, kubadilishwa au kuhaulishwa kielektroniki, kupiga chapa, kurudufiwa au kurekodiwa kwa utaratibu wowote ule katika hali yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa Mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, Fortunata Moses Kabeja, ninakiri kwamba tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na kwamba kazi hii hajjawaasilishwa katika chuo kingine chochote kwa tuzo yoyote.

.....

Saini

.....

Tarehe

TABARUKU

Kazi yangu hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu Baba yangu Mzee Claudio Wakusongwa na Mama yangu Consolata Joseph Wakafumbe kwa malezi mema na kunisomesha.

Msimamizi wangu Prof. Dkt. Sheikh TS. Y. M. Sengo na wapenzi wote wa lugha ya Kiswahili.

SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati nazitoa kwanza kwa mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na Afya nzuri. Matunda na mafanikio ya kazi hii yametokana na jitihada, Elimu, Ushauri na misaada mbalimbali niliyoipata kutoka kwenye taasisi na watu mbalimbali. Kwa unyenyekevu mkubwa natambua msaada na mawazo ya watalamu wa Lugha ya Kiswahili.

Pili natoa shukrani zangu za kipekee kwa msimamizi wangu wa shahada hii Prof., Dkt. Sheikh T.S.Y M.Sengo wa chuo kikuu huria cha Tanzania ambaye kwa muda wote amekuwa akinishauri, kunielekeza, na kupitia kazi zangu kwa upendo mkuu wenye taalimu za lugha ya Kiswahili kuanzia hatua ya awali ya uundaji wa pendekezo la utafiti, ukusanyaji, uchambuzi wa data mpaka kufikia hatua ya mwisho ya uandishi wa tasnifu hii.

Tatu napenda kutoa shukrani zangu kwa mume wangu Moses Kabeja, watoto wangu Kabesi, Denis, Doris, David na Edwin kwa msaada na uvumilivu walionesha wakati wote wa kufanya kazi hii kwani ilihitaji kusafiri na kwenda kufanya tafiti maeneo mbalimbali ambapo pia nilitumia muda na fedha na kuwacha wakiwa wapweke bila mapenzi na malezi ya mama.

Nne natoa shukrani zangu za dhati Kwa mwajiri wangu ambaye ni mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Ndugu Daudi Mayeji kwa kuniruhusu kusoma na kunipa misaada mbalimbali ya hali na mali.

Tano natoa shukrani za dhati kwa walimu wangu wa chuo kikuu huria cha Tanzania kituo cha Arusha chini ya mkurugenzi wa kituo mama Saria kwa kuniunga mkono na

kunipa moyo wa kujiendeleza tangu shahada ya kwanza hadi hatua hii kwa ushirikiano na Mkurugenzi wa kituo Chuo Kikuu huria Dodoma.

Sita naomba shukrani zangu ziwaendee walimu wa Kiswahili katika Seckondari za Mkoa wa Dodoma, vyuo vikuu vya Mtakatifu Yohana na Chuo kikuu cha Dodoma, Tanga Sekondari na Mkurugenzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Tanga.mama Felistas, Richard Mahonge, Ndugu, jamaa, viongozi na marafiki wa Marehemu shaaban Robert walioko Machuni Tanga, Handeni na Dar es salaam wakiongozwa na mtoto wa kiume wa shaabani Robert aitwaye IKBAL.

Saba napenda kuwashukuru watu mbalimbali walioniwezesha kwa kunihifadhi, na ambao wametoa mali na vifaa vya kunisaidia ni pamoja na familia ya Charles Wakusongwa (marehemu) Bwana Mangesho katibu chama cha walimu mkoa wa Tanga, familia ya Bwana Mfaume wa Segerea DSM, familia ya Bwana na Bibi Richard Mazinge wa Dar es Salaam, mkurugenzi na watumishi wote wa chuo cha mifugo na utafiti Mpwapwa, Familia ya Marehemu Sheikh Mkuu wa Mpwapwa aitwaye Sheikh Ally Khamisi Liembe, pamoja na Mzee Joseph Mbeho aliyekuwa rafiki wa marehemu Shaban Robert kwa kunipokea wakiwa pamoja na Mzee Ngoma Msalange kwa pamoja walinielegeza na kunitembeza maeneo yote aliyofanyia kazi na kuishi marehemu Shaaban Robert wakati akiwa Mpwapwa kama Mtumishi yaani karani wa forodha katika kituo cha utafiti wa mifugo Mpwapwa.

IKSIRI

Tasnifu hii imejaribu kuchangia mawazo na fikra za jinsi ya kutumia fasihi ya lugha katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa kupitiya fani ya ufutuhi. Dhima ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert imeathiri wasomaji, watunzi na wapenzi wa lugha ya Kiswahili kwa kiwango cha juu sana. Sura ya kwanza inatoa utangulizi wa ujumla historia ya marehemu Shaaban Robert, maisha yake, familia yake, kazi na ajira zake, mbari zake kwa ujumla na kazi zake za fasihi alizofanya. Sura ya pili inaelezea mawanda yakinadharia, mkabala wakinadharia ambao umetoa mchango katika kazi hii yaani nadharia tete na nadharia kiongozi. Sura ya tatu ni tahakiki za kazi mbalimbali zilizotangulia ikielezea kazi mbalimbali kuhusu ufutuhi na Dhima ya ufutuhi pamoja na maudhui yake katika Riwaya zilizo lengwa. Sura ya nne inafafanua mbinu za utafiti ambazo zimetumika ikiwa ni pamoja na umakinifu, usaili na hojaji. Sura ya tano imewasilisha matokeo ya utafiti. Yanaonesha kuwa uhai wa fasihi ya Lugha unategemea ufundi na umakini wa mpangilio wa maneno. Kiini ikiwa ni dhima ya ufutuhi ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Kutokana na kukua kwa lugha ya Kiswahili na uwanda wake mpana wa fasihi imeonesha wazi kuwa, Dhima ya ufutuhi ni muhimu sana katika fasihi ili kuamsha ari na kuleta mvuto wa Lugha ya Kiswahili hususani katika kizazi hiki kilichopo. Hatimaye ni hitimishi na mapendekezo yaliyotolewa kama vile kuhimiza misingi bora ya ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili, mbinu shirikishi za dhima ya ufutuhi kulingana na wakati uliopo na kuhamasisha jamii na Taifa letu kuipenda na kuithamini lugha ya Kiswahili kama Lugha ya Taifa. Kusoma vitabu vyake Shaaban Robert, kuzuru maeneo ya asili yake na kuviingiza vitabu vyake katika mtalaa wa Elimu na somo la Kiswahili kwa ngazi zinazohusika.

YALIYOMO

UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI	ii
HAKIMILIKI.....	iii
TAMKO LA MTAHINIWA	iv
TABARUKU.....	v
SHUKRANI.....	Error! Bookmark not defined.
IKSIRI.....	viii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xii
ORODHA YA VIFUPISHO.....	xiii
SURA YA KWANZA.....	1
1.0 UTANGULIZI WA JUMLA.....	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Utangulizi Unaendelea	2
1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti	3
1.5 Nia Kuu ya Utafiti.....	22
1.6 Madhumuni Maalumu ya Utafiti.....	22
1.7 Maswali ya msingi ya utafiti	23
1.8 Umuhimu wa Utafiti.....	23
1.8.1 Matokeo ya Utafiti.....	24
1.9 Eneo la Utafiti.....	26
1.9.1 Eneo	26
1.9.2 Mipaka ya Utafiti	26
1.9.3 Ukubwa wa Uteuzi.....	27

1.9.4 Uteuzi wa Walengwa	27
1.9.5 Upatikanaji wa Uteuzi.....	27
1.9.6 Makundi ya Uteuzi Kijinsi.....	29
1.9.7 Eneo Lililoongezwa	29
1.9.8 Sababu za Kufanya Utafiti Katika Eneo Hili	29
1.9.9 Matatizo Vikwazo / Utatuzi	29
SURA YA PILI.....	31
2.0 MKABALA WA KINADHARIA	31
2.1 Utangulizi.....	31
2.2 Nadharia Mbalimbali	31
2.2.1 Nadharia ya Utafiti	31
2.2.2 Nadharia ya Mtu -Utu	33
2.2.3 Nadharia ya Dini na Mtu Binafsi	35
2.2.4 Nadharia ya Fasihi na Jamii	36
2.2.5 Nadharia ya Uasilia.....	36
2.2.6 Nadharia ya Ndani –Nje.....	37
2.3 Nadharia Tete	42
2.4 Nadharia Kiongozi	43
SURA YA TATU	45
3.0 KAZI TANGULIZI.....	45
3.1 Utangilizi	45
3.2 Tahakiki za Kazi Tangulizi	46
SURA YA NNE.....	49
4.0 MBINU NA NJIA ZA UTAFITI.....	49

4.1	Usuli wa Kuingia Masikanini	49
4.2	Mbinu za Kukusanya Data	50
4.2.1	Dhana ya Mbinu Za Kukusanya Data.....	50
4.2.2	Umakinifu	51
4.2.3	Usaili.....	51
4.2.4	Hojaji	51
4.2.5	Wasaidizi Katika Kukusanya Data	51
4.3	Zana za Utafiti	52
4.5	Bajeti	52
	SURA YA TANO	54
	5.0 UCHAMBUZI WA DATA	54
5.1	Utangulizi.....	54
5.2	Madhumuni ya Kiini cha Uchambuzi wa Data	54
5.3	Uchambuzi wa Data	54
5.4	Aina ya Data.....	55
5.4.1	Data za Msingi	55
5.4.2	Data za Upili	55
5.5	Uwasilishaji wa Data	56
	SURA YA SITA.....	60
	6.0 MHUTASARI NA MAPENDEKEZO	60
6.1	Muhtasari	60
6.2	Mapendekezo	62
	MAREJELEO	65
	VIAMBATISHO	75

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1.1: Kuonesha Upatikanaji wa Uteuzi.....	27
Jedwali Na. 1.2: Kuonesha Makundi ya Uteuzi Kijinsi.....	28
Jedwali Na. 5.1: Kuonesha Takwimu za Majibu ya Watafitiwa.....	56
Jedwali Na. 5.2: Maswali ya Utafiti.....	57
Jedwali Na. 5.3: Kuonesha Majibu ya Watafiti wa Juu ya Swali Na.3 (Athari za Dhima ya Ufutuhi).....	59

ORODHA YA VIFUPISHO

Bw	-	Bwana
Dkt	-	Daktari
Dhana	-	Kudhani/kuhisi
MA	-	Master of Arts
ME	-	Mwanamume
NA	-	Namba
KE	-	Mwanamke
JML	-	Jumla
MWL	-	Mwalimu
N.K	-	Nakadhalika
Prof.	-	Profesa
SR.	-	Shaaban Robert
Tsh	-	Shilingi za Kitanzania
UK	-	Ukurasa
OALD	-	Oxford Advanced Learners Dictionary

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Miongoni mwa wanazuoni Maarufu wa Lugha ya Fasihi ya Kiswahili wanaokumbukwa Afrika Mashariki ni pamoja na Marehemu Shaaban Robert. Kwa wapenzi wote wa lugha ya Kiswahili humkumbuka sana kutokana na mchango wake kwa lugha hii, kazi zake mbalimbali kama Riwaya na ushairi ni kioo toka kwa jamii yote ipendayo na kutumia Lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla kazi zake zimejaa kila aina ya ufundi na vionjo mbalimbali vya Lugha. Hivyo vyote vinavyomfanya mtunzi Marehemu Shaaban Robert aitwe gwiji, bingwa na mahili wa lugha ya Kiswahili.

Shaaban Robert alizaliwa tarehe 1 Januari mwaka 1909 huko vibambani Tanga. Alipata Elimu ya msingi katika shule ya msingi Kichwele (sasa Uhuru mchanganyiko Dar es Salaam). Baada ya kumaliza darasa la nane aliajiriwa na kufanya kazi sehemu mbalimbali kama ifuatavyo:

Aliajiriwa na serikali ya kikoloni kwa mara ya kwanza kama karani wa kodi huko Pangani mwaka 1926-1944, karani wa ushuru wa Forodha Afisi ya mkuu wa Jimbo Tanga mwaka 1946-1952. Afisa wa kipimo Ardhi nchi tangu mwaka 1952-1960 (Idara ya Ardhi), Mwalimu Old Tanga Sekondari Karani Chuo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa Dodoma 1960. Kati ya kazi zake nyingi alizowahi kutunga na kuandika ni pamoja na Riwaya za Kusadikika, Kufikirika, Siku ya Watenzi Wote na Adili na Nduguze. Hizi ndizo Riwaya ambazo mtafiti atazichambua na kuainisha ujumbe, fikra tamaduni na uushahaji wa Lugha ya Kiswahili, utunzi na mantiki ya uteuzi wa walengwa kwa ujumla wake.

1.2 Utangulizi Unaendelea

Wataalamu wengi wa fasihi ya Lugha ya Kiswahili wameandika kazi nyingi na kuzisambaza ili ziweze kusomwa, Lakini kazi za Shaaban Robert zinatakiwa kupewa umuhimu wa kwanza ili zionwe na uzuri wa kipekee ulio na uwezo na mvuto mkubwa katika jamii ya Kitanzania na dunia nzima. Vigezo na mambo muhimu ambayo yanachangia kwa kiasi kikubwa kufanikiwa kwa watunzi wa kazi ya fasihi katika kuwasilisha maudhui ya kazi, ni uundaji mzuri wa fani, kuwepo kwa urari na muwala baina ya fani na maudhui katika kazi yoyote kuhusisha fasihi ya lugha, hurahisisha kuwepo kwa upogo na kuelewa baina ya matokeo halisi ya kazi na kiwango cha kuelewa ambacho hadhira hukipata (Senkoro 1982).

Chimbuko la kazi zozote za mtunzi wa Fasihi ni lazima awe na wazo lake moyoni, ambapo huamua kulisema kwa kutumia maumbo na mitinndo tofauti. Fani ni sehemu muhimu ili kufanya maudhui ya kazi za fasihi yawafikie hadhira kwa wepesi zaidi. Kazi za marehemu Shaaban Robert zimeonesha umahili na mvuto mkubwa sana kwa wasomaji wake ni kwa sababu ya kupitia kipengele cha Fani.

Sengo.1975, Senkoro, 1987, Wamatila, 2002 juhudi na uwezo wa kufanya kazi nzuri ya Fasihi husababisha walengwa wa kazi ya Fasihi kupata thamani halisi ya kazi ya mtunzi alivyowaza na kujiwekea malengo.

Shaaban Robert ni miongoni mwa waandishi na watunzi maarufu wa kazi za fasihi ya Kiswahili. Mwandishi huyu amejizolea umaarufu kupitia kazi zake za Riwaya na ushairi. Umaarufu wake umekithiri viwango vya kawaida na hatimaye kufananishwa na Gwiji la Fasihi ya Kiingereza aitwaye Shakespeare (lonly.1981-1977).

Ufutuhi ni njia ya kufikisha ujumbe kwa haraka na unaamsha ari na utafiti katika kupata maudhui ya ujumbe.

1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Usuli wa tatizo la utafiti huu umetokana na msukumo nilioupata ambao unaonesha upungufu katika uundaji mzuri wa fani, kuwepo kwa urari na muwala baina ya fani na maudhui, kurahisisha kueleka kwa ujumbe kukosekana kwa urari husababisha kuwepo kwa upogo wa kuelewa baina ya matokeo halisi cha kuelawa ambacho hadhira hukupata (Senkoro, 1982).

Pili: Kazi za Shaaban Robert zimebainika kuwa na mvuto mkubwa kwa wasomaji hivyo nimejikita katika kuongeza ari ya usomaji kwa kujikita katika kuchambua nafasi na dhima ya ufutuhi katika kazi zake ili kuongeza wigo wa utafiti na udadisi

Tatu: wachambuzi wengi wa kazi za Shaaban Robert wamejikita katika kuchambua kazi zake lakini kipengele cha nafasi ya wakuza mtaala ni finyu katika kuboresha muuhtasari.

Mtunzi yeyote wa kazi ya fasihi huwa na wazo lake moyoni, ambapo huamua kulisana kwa kutumia maumbo na mitindo tofauti. Fani ni sehemu muhimu sana ilikufanya mudhui ya kazi ya fasihi yawafikie hadhira kwa wepesi zaidi. Kupitia kipengele cha fani, marehemu Shaaban Robert ameonesha umahili wake katika kuifanya kazi zake za fasihi kuwa na mvuto kwa wasomaji.

Senkoro, 1987, Sengo 1975 na Wamatila, 2002, wanasema, juhudi na uwezo wa kufanya kazi nzuri ya fasihi, husababisha walengwa wa kazi zake za fasihi kupata thamani halisi ya kazi ya mtunzi kadri alivyowaza na kulenga.

Katika orodha ndefu ya waandishi maarufu kupitia kazi zake za ushairi na Riwaya. K (Mbuguni, 1978, Sengo, 1975, Momanyi, 2001). Mazingira hayo ya upekee katika maandishi hutokana na umahili wake katika uwanja wa uandishi, amefikia hatua ya kufananishwa na Shakespeare ambaye ni Gwiji la fasihi ya Kiingereza (Only, 1981:1977).

Hata hivyo Shaaban Robert anajipambanua na kujichomoza sana kati ya waandishi wengine wa kazi za fasihi ya Kiswahili kupitia upekee wake katika uteuzi wa maneno na matumizi ya lugha na mbinu zenye ubunifu mwingi. Miongoni mwa vipengele vya pekee vinavyojiokeza katika kazi zake ni *matumizi ya ufutuhi* na *uundaji* wa mandhari ya *kitopia* Upekee huo hufanya msomaji ahitaji umakini mkubwa ili kuelewa maudhui yake ya Shaaban Robert, matokeo ya umahili huo ni kuwepo kwa wataalam kadhaa waliojitokeza kuyatafiti, ili kuelewa maudhui yake (Mbuguni, 1978, Sengo1975, Momanyi 2001).

Aidha mimi kama mtafiti niliyemchagua Shaaban Robert nimevutiwa na matumizi ya ufutuhi pamoja na uundaji wa maneno katika kazi mbalimbali za mwanazuoni huyo. Nimebaini pengo lililopo kati ya wasomi wa lugha ya Kiswahili jinsi wanavyo unda na kutumia ufutuhi katika kufikisha ujumbe ni mbinu zilizofikirisha vya kutosha.

Mfumo na muundo wa uandishi wa kazi za Shaaban Robert unaofikirisha na kuleta shauku ya usomaji ndio ulionishawishi kumchagua na kuteua kipengele cha dhima ya ufutuhi katika kazi zake zinavyojitokeza ili nizichambue kupitia vitabu vinne ambavyo ni kusadikika, kufikirika, siku ya watenzi wote na Adili na Nduguze.

Uteuzi wa washiriki na majina yote yaliyotumika katika vitabu hivi ni viwakilishi vya kutosha kufikisha ujumbe ingawa takribani vyote ni vya kubuni au kudhaniana au kufikirika tu. Ili msomaji aweze kupata Dhana halisi ni lazima afikiri na kuzama katika kutafakari utunzi huo kwani ujumbe ni fiche. Nimebaini kuwa baadhi ya vipengele vya maandishi ya Shaaban Robert vimeshughulikiwa kwa mtazamo wa jumla au vimeondolewa tu au vingine havikushughulikiwa kabisa

Dhima ya ufutuhi ni kipengele nilichochagua kufanyia utafiti zaidi ili kuwasaidia wasomaji kupata Dhana tarajiwa, kusanifiwa na kuhifadhi matokeo ya tafiti hizo kwa lengo la kukuza kuhifadhi na kuwatangaza malenga wetu hususani marehemu Shaaban Robert. Wapo wataalamu wengi waliowahi kushughulikia maandishi ya Shaaban Robert.

Wafuatao ni baadhi ya wataalamu waliyowahi kuyashughulikia maandishi ya Shaaban Robert; Kezilahabi (1976), riwaya kwa kutazama maudhui kwa ujumla wake; Gibbe (1978) na Ndulute (1994), maandishi ya Shaaban Robert yanayohusu ushairi. Sengo na Kiango (1973), wamezichambua baadhi ya riwaya zake. Sengo (1982) amejishughulisha na uchambuzi wa riwaya ya Shaaban Robert ya Siku ya watenzi Wote na (1975) kuchapisha kitabu cha Shaaban Robert: *Uhakiki wa Maandishi Yake*.

Maandishi wengine waliandika juu ya futuhi na kusimamia kazi za fasihi ni Prof. Emmanuel Mbogo katika vitabu vyake Morani (1996), Watoto wa Mamantilie (2000), Giza limeingia (1988) Tone la mwisho (1996). Ijapokuwa wataalamu hawa na wengine waliofanyia kazi maandishi ya Shaaban Robert, wamefanikiwa katika kuibua ari ya kuzisoma kazi zake na kuzielewa, bado kipengele cha Ufutuhi katika

maandishi yake pia kimeshughulikiwa na mtafiti mahiri ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kuu cha Dodoma Athuman Ponella. Yeye katika tasnifu yake ya Nathari za ufutuhi katika kazi za Shaaban Robert aliyofanya mwaka 2007 ametafsiri maana ya ufutuhi na kama nilivyo mtafsiri yeye anajumuisha kuwa ufutuhi ni vichekesho na ufutuhi ni fasihi inayotumika na inayotoa ujumbe kwa njia ya vichekesho pia inaamsha ari ya utafiti katika kupata ujumbe unaokusudiwa. Pamoja na tafsiri za waandishi mbalimbali mimi najumuisha kuwa ufutuhi ni sanaa ya kifasihi inayotengemea vipengele kama mazingira, maumbile, uonekanaji na aina ya hadhira katika kufikisha ujumbe.

Aidha nimeona bado upo umuhimu wa kufanya utafiti zaidi kwani kpengele hiki cha ufutuhi kinahitaji kushughulikiwa zaidi na kuchambua dhima yake katika sanaa. Kipengele cha Ufutuhi katika maandishi au Riwaya za Shaaban Robert nimekifanyia uchambuzi kwa makini na kuchambua Riwaya nne ambazo ni Siku ya Watenzi Wote, Kusadikika, Kufikirika na Adili na Nduguze.

Matumizi ya ufutuhi katika riwaya za mtunzi Shaaban Robert nyingi zimetumika kama sehemu fiche za kufikisha ujumbe. Ufutuhi katika kazi hizi zote nne nilizoteua umejitokeza katika matumizi ya lugha, lengo au maudhui tarajiwa, uteuzi wa maneno, uteuzi wa washiriki, wadhifa wa wateule na matokeo ya utunzi.

Siku ya watenzi wote ni Riwaya ya Shaaban Robert yenye kufikirisha na inayotoa mwongozo kwa waanadamu namna ya kuhusiana wao kwa wao na baina yao na Mwenyezi Mungu. Matumizi ya ufutuhi katika Riwaya hii yanajibainisha katika sura ya kwanza hadi sura ya kumi na nne.

Mfano katika sura ya kwanza inayohusu mabadiliko Shaaban Robert ameandika utenzi mfupi wa “kichaka” Nukuu yake ni kama ifuatavyo.

Kichaka hiki kizuri,
Kwa marashi na uturi,
Harufu yake si nzito,
Kwa tamu ya manukato.

Ndege huyu anayesifia kichaka hiki kwa sababu humpa hifadhi ya usiku na asubuhi yake ndege huyohuyo hugeuka akaimba kashifa kutwa:

Kichaka hiki kichafu,
Kwa uvundo wa harufu,
Ya gugumo na kutuzi,
Na ubaya wa pumzni.

Katika riwaya hii nimebaini ufutuhi katika mpangilio wa Lugha na matumizi ya kashifa katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Pia inaonesha jinsi mtu anavyoweza kuwa mnyenyekevu anapokuwa na shida lakini anapotimiziwa shida au mahitaji yake husahau na kupuuzwa wema wote aliotendewa hatimaye kutoa kashifa kama ilivyo katika sehemu ya pili ya utenzi huo. Ndege amefurahisha na kushangaza wasomaji kwa tabia hizo ingawa ndiyo ufutuhi unapojitokeza.

Katika sura ya tatu inayohusu “sadaka” Shaaban Robert amesisitiza umuhimu wa kutoa sadaka kwa watu wote hususani walio maskini. Pia mtunzi amebainisha watu wamchao Mungu sana wanaonekana kuwaamini watu wa dini wanaotoa Zaka, kumbe mali hizo zimeokotwa mfukoni mwa maskini kila kitu kwa rehani zilizokuwa

hazikomboleki, fasihi za mchanganyiko na upotovu wa maisha. Wengine utajiri wao umetokana na unyang'anyi, ufidadi na dhuruma kadhaa, Shaaban Robert ametunga riwaya hii katika ukurasa wa 27:

Wa angani

Ndiyo ndege warukao

Wenye dini

Ndiyo nyoka waumao

Ufutuhi hapa unabainisha watu wema na wanafiti wanaofananishwa na nyoka waumao. Shaaban Robert amediriki kusema kuwa hili neno ambalo hapana mmoja kati yetu mwenye hakika ya kutosha juu yake; Hali kaumu ya watu ina tuhumu kama hizi.

Ufutuhi mkubwa umetumika katika Riwaya hii imebainisha watu wanaoonekana wema mbele za binadamu kwa kutoa sadaka na michango mbalimbali tena yenye mashiko mazito katika nyumba za ibada huku masikini wakiachwa bila kutambulika na kunyanyaswa kutokana na michango yao duni. Hawa ndege wa angani wanawakilisha matajiri wenye usemi katika dini na wale masikini wamchao Mungu bila mali yoyote ndiyo nyoka waumao kwa maana ya kwamba jamii haiwatambui na mchango wao mdogo hauna mashiko hivyo huishia kudharauliwa na kupuuzwa, ndiyo fasihi ya wenye dini ndiyo nyoka waumao inavyotoa ujumbe. Ufutuhi hapa umelenga katika misemo, viwakilishi ambavyo vinatoa Dhana nzima ya maadili mema.

Mfano katika sura ya kumi na tatu inayohusu Riba, Shaaban Robert ameonesha pengo kubwa liliopo kati ya matajiri na masikini. Ameonesha jinsi wenye mali

nyingi matajiri wasivyo kuwa tayari kusaidia masikini. Mfano ni pale ambapo yule tajiri alichukua masufuria ya mwanamke masikini kwa kumwekea riba kubwa iliyosababisha yule mama maskini kushindwa kuyakomboa na kushindwa kulisha watoto wake.

Katika sura hii pia Shaaban Robert ameonesha tofauti au pengo lililopo kati ya wanaume na wanawake na unyanyasaji unafavyofanywa na wanaume wakatili kutumia rasilimali za familia kwa anasa nje ya ndoa. Aidha mwandishi katika sura hii ameonesha matumizi ya nguvu na ubabe wa wanaume kwa wake zao. Shaaban Robert ametumia ufutuhi katika kueleza usawa wa binadamu na haki za wanawake na watoto katika jamii kuwa ni lazima ziheshimiwe.

Katika sura ya mwisho ya kumi na nne ya Fungate ufutuhi umejitokeza katika kuonesha umuhimu wa maadili mema, kumcha Mungu na utaratibu wa kupata mchumba mwema na vilevile ameweka msisitizo juu ya adhimisho la ndoa na Fungate ya furaha na mapenzi ya maisha yenye amani na upendo milele. Shaabani Robert amesema mke ni thawabu na dhahabu. Mume ana wajibu na sahibu licha ya kuongelea mapenzi katika sura hii.

Shaaban Robert amesisitiza umuhimu wa wazazi au walezi kuandika wosia na kugawa mirathi kwa wanafamilia kwani inapunguza lawama na kuleta amani na utulivu kwa wanafamilia, mfano Sara na Ayubu ndoa yao imetokana na wosia alioacha marehemu shangazi yake Ayubu aliyeitwa binti Akili. Pia amesisitiza kumcha Mungu na kumtolea sadaka. Huu ni ufutuhi.

Dhima ya ufutuhi katika Riwaya ya Shaaban Robert katika siku ya watenzi wote duniani inafanya msomaji kufikiri sana ili kupata Dhana inayolengwa. Pia riwaya hii itamfaa yoyote anayependa kujua mawazo na falsafa ya maisha ya Shaaban Robert kuhusu ulimwengu ndiyo maana amehitimisha Riwaya hii kwa kusema:

“Tamati natia mwisho kuwahadithia shani,
Hadithi ya furahisho kwa jamii duniani,
Kuwa kama makumbusho ya mtunzi Shaaban”.

Mwisho wa kunukuu.

Katika Riwaya ya Kufikirika, Shaaban Robert amejikita katika matumizi makubwa ya ufutuhi ili kuwasilisha ujumbe uliomo ndani yake. Kwanza kabisa kufikirika ni nchi ya kubuni ambayo inaonekana katika fikra kuwa ni nchi kubwa katika nchi za Dunia, Kaskazini imepakana na Anasa, Kusini imepakana na nchi ya Majaribu, Mashariki Bahari ya Kufaulu na Magharibi safu ya milima ya Jitihadi. Njia ya kwenda nchi hii hukanyagwa kwa fikra tu siyo nyayo.

Wafikirika ni wengi nao ni wazazi mno. Shaaban Robert ameiwasilisha nchi ya Kufikirika kuwa yenye watu wengi wema wenye maisha bora na raha tele ingawa kuna maradhi na vifo. Ni nchi inayotawaliwa na nasaba kubwa sana ya wafalme ambao waliungana kwa vizazi kama viungo vya mkufu, Mfalme wa mwisho kutawala nchi hii alichelewa kupata mtoto wa kurithi. Hivyo Riwaya hii imesheheni visa, mikasa, simulizi na kuonesha umuhimu wa kila mtu katika maisha na jinsi wanadamu wanavyopaswa kusaidiana katika shida mbalimbali. Mfalme wa Kufikirika katika sura ya kwanza ameonsha pengo kubwa lililopo kati ya watu wa

kada ya chini na matajiri lakini wanavyoweza kuwa na amani endapo watajaliwa kuzaa watoto.

Mwanamke ametafsiliwa kama kiumbe mwenye busara, hekima, upendo na uvumilivu katika malezi ya familia. Shaaban Robert ametumia neno wivu kama silaha ya kuleta mafanikio katika jamii, majeshi shupavu, viongozi shujaa, raia wengi na wema, amesema jina lake litachorwa kwa majohari Ameonesha umuhimu wa kupata mtoto, kulea mwana na mtoto wa wakufikia ni sawa na kununua bidhaa sokoni na mwana aliyenunuliwa anakuwa sawa na mtumwa si muungwana wala si mtoto kwa mnunuzi wake.

Mfalme anadai kuwa anataka mtoto asiye mtumwa anasisitiza kuwa ugumba umemeza heshima yake na utasa umetia vumbi fahari ya malkia wake. Mfalme wa Kufikirika anamtafsiri mtoto kuwa mrithi, mshauri, mtawala na mwongozaji ndani ya falme na jamii. Riwaya hii imeonesha umuhimu na tabibu na wataalam wa tiba mfano waganga wa kutibu kupiga ramli ambao wamegawanyika katika makundi muhimu ya waganga wa mizizi, makafara, mazinguo, hirizi, mashetani, waganga na watabiri hawa wote warishirikishwa ili kupambana na methali isemayo nyumba ya mgumba haina matanga. Huu ni msisitizo wa mfalme kupata mtoto wake mwenyewe.

Katika sura ya pili mtunzi anasema “Hamu ya mtawala wa mazuo yote ametumia usemi huu kubeba ujumbe muhimu kuwa hamu ndiye chimbuko la watu kufanya kazi kwa bidii, na kukidhi mahitaji. Matokeo ya kazi na jitihada kubwa za kuajabisha zilifanywa na watu wa Kufikirika wakati wote. Hivyo kila mtu alisisitizwa kufanya kazi kwa bidii ili kuleta ustawi katika jamii”.

Jitihada za waganga zilizaa matunda pale ambapo kundi la waganga watabiri liliposhinda na hatimaye Malkia akazaa mtoto wa kiume. Sehemu ya shairi la Mfalme ni kielelezo cha ufutuhi kama ifuatavyo:

Mfalme na Malkia
 Katika Kufikirika
 Siku ya kuzaliwa
 Mtoto tuliyemtaka
 Wote tumependezwa
 Mtabiri twataka
 Makumbushoni kutiwa
 Watu kukumbuka
 Jina lake milele
 Lazima likumbukwe
 Kama watu wateule
 Na yeye anakiliwe
 Nchi ijae tele
 Watu mfano wa yeye
 Daima kwenda mbele
 Mambo yatazamwe
 Jina lipewe wana
 Kulikariri kwa moyo
 Waelezewe maana
 Wakuze wayatendayo
 Kama mlivyoona

Matendo ya mtu huyo

Katenda bora sana

Kwa tuzo apewayo

Kushuhudia dhahiri

Kaziye kuwa bora

Jina la mtabiri

Kwa herufi lang'ara

Tofauti za johari

Herufi kila sura

Mtu mashuhuri

Mpangilio wa maneno, misamiati na viwakilishi ni matumizi dhahiri ya ufutuhi katika riwaya hii na usemi kama ufuatao **Utu Busara Ujinga Hasara** umefafanua jinsi ambavyo binadamu anaweza kutanguliza utu na kuona ujinga kama chimbuko la madhara katika maisha. Mfalme wa Kufikirika ameonsha mwamko Mkuu juu ya Elimu ingawa imani yake kwa walimu ni haba, mwalimu na mwanafunzi wake yaani mtoto wa mfalme wameonesha mahusiano bora mfano, katika ukurasa wa 26 katika kitabu hiki cha Kufikirika Mwalimu na Mwanafunzi wanasema.

“Matengano yanauma

Baki ni kuvumilia”

Mfalme ameona kazi ngumu ya ualimu kama kazi rahisi ambayo anaweza kufanya mtu yeyoye ndiyo maana amebadilisha waalimu wa mtoto wake bila kupima uwezo wao. Ufutuhi unajitokeza zaidi pale wajumbe wanaoamua sheria ya kutoa makafara na kumwaga damu, kupitishwa na kuteketezwa. Baada ya mvutano wanasema

maisha ya uongo ni mafupi. Watu wavaao uongo kama lebasi ghafla hujiona hawana nguo mbele za wenzao.

Mfano katika utenzi ufuatao:

“Kweli kama lebasi

Uongo nao matusi

Tena kweli almasi

Kitu hazizi halisi

Uongo pia najisi

Mtu mwema haugusi

Riwaya ya Kufikirika imejumuisha matumizi mbalimbali ya ufutuhi ambayo yanafikisha ujumbe kwa jamii kwa lugha fiche. Mfano katika sura ya mwisho ukurasa wa 49 yapo maneno na Sentensi zinazojumuisha matukio na visa zote zinatoa ujumbe mfano, “Jitihada ina tuzo siku zote. Matendo yako bora uliyoyatenda hustahili heshima kubwa sana”. Mtunzi mahiri Shaaban Robert ni mweledi na mpangilio wa matunzi ya ufutuhi katika riwaya hii ya kufikirika inaleta hamasa na kuibua ari ya usomaji na kuongeza udadisi na ubunifu miongoni mwa wasomaji wa vitabu vya Kiswahili.

Riwaya ya Kusadikika iliyoandikwa na Shaaban Robert inatuelekeza katika nchi ya Kufikirika kimawazo tu. Nchi hii iko katikati ya mipaka sita. Kaskazini imepakana na upepo wa Kaskazini, Kusini imepakana na upepo wa Kusini, Mashariki imepakana na Matlai na Magharibi imepakana na upepo wa umande. Mipaka miwili mikuu ni: Kwa juu nchi hiyo inepakana na mbingu na chini imepakana na Ardhi. Wanawake wote katika nchi ya Kusadikika huzaa mapacha.

Taswira ya jumla juu ya Kusadikika ni kwamba ni nchi yenye maajabu makubwa na ina watu au wakazi waliojaa visa mbalimbali; Dhima ya ufutuhi katika Riwaya hii ya Kusadikika imejitokeza kuanzia Sura ya kwanza mashtaka, pili uwanasheria, sura ya tatu mjumbe wa Kaskazini, sura ya nne mjumbe wa Mashariki sura ya tano mjumbe wa Kusini, sura ya sita mjumbe wa Magharibi, sura ya saba mjumbe wa mbinguni, sura ya nane mjumbe wa ardhini, sura ya tisa Hukumu.

Katika sura ya kwanza lugha inayotumika kumtambulisha waziri wa Kusadikika ni kwa kutumia maneno machache sana lakini yakipambanuliwa yana maana pana zaidi. Mtunzi anasema waziri wa kusadikika alikuwa mtu mwenye haiba kubwa na uhodari mwingi kwa hivi alitwa Majivuno. Kifungu cha maneno katika sura ya kwanza dhidi ya mshitakiwa Karama kutoka kwa waziri Majivuno kuwa tone moja la maji haliwezi kuleta gharika katika nchi, inamaana ya kumdharau Karama na kwamba uwepo wake katika jamii hauna thamani kubwa.

Katika ukurasa wa nne Aya ya kwanza mtunzi anasema “mikono ya Mashtakiwa ni mifupi kwa kutenda wema wowote. Kwa hali hii nachelea kuwa akiamriwa kuinyoosha katika matendo makubwa matokeo yake yatakuwa machafuko, uasi na maangamizi Mchwa ukikaribia kuangamizwa hufanywa kumbikumbi na kuoteshwa mabawa mawili utaalumu huu wa lugha unabeba nafasi ya matumizi ya ufutuhi katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ujumbe uliosheheni katika vifungu hivi unatosha kumwelezea mlengwa kuwa yeye si mtu maarufu sana lakini anao uwezo wa kutumia mbinu mbalimbali zenye hila katika kujinasua na kushawishi jamii dhidi ya Serikali iliyoko madarakani. Mchwa na kumbikumbi ni wadudu wanaooneesha

ushirikiano mkumbwa katika maisha yao. Nguzo yao kuu ni kujituma na kushirikishana.

Matumizi ya maneno kama kipawa lenye maana ya kipaji au uwezo mkubwa zahili maana yake ni Mwenyezi Mungu, taratibu ni mpangilio au mifumo, upelelezi ni utafiti, ufuatiliaji wa siri au upekuzi wa habari au matukio, kuvutana ni kutofautiana katika maamuzi au msimamo haya ni baadhi ya maneno ya kifutuhi yaliyotumika katika sura ya kwanza,

Katika sura ya pili mtunzi anasema kuwa “msiba wa kujitakia hauna kilio”. Tafsihi yake ni kwamba mtu anaposhauriwa, kukatazwa na kuonywa juu ya jambo fulani na akikaidi, endapo atapata madhara au hasara lawama zote humwelekea mtendaji. Mfalme wa Kusadikika anasema kitanda usicholalia huwajui kunguni wake. Ni dhahiri kuwa uzito wa kazi aifanyayo mwenzio siyo rahisi kuifahamu waweza kudharau kumbe ni mzigo mzito.

Waziri wa Kusadikika aitwaye Majivuno alikusudia kumtosa mshtakiwa Karama katika bahari ya maangamizi ina maana kuwa baadhi ya watawala hutumia vyeo na uwezo wao wa utawala na sheria kuwakandamiza raia hata kama hawana hatia. Yaani unyanyasaji na matumizi mabaya ya mamlaka au madaraka. Kati ya sura ya pili hadi sura ya tisa yapo matumizi kadha wa kadha ya ufutuhi mfano. Ukurasa wa 19 aya ya pili mtunzi anasema ushujaa ni husuni kubwa na hazina bora ya kudumishwa. Zipo namna mbili za ushujaa kwanza ni ushujaa wa nguvu na nasaha ambapo wanadamu hupata amani ya daima.

Katika kuonesha misingi ya utawala bora Shaaban Robert anasema habari za mamlaka ya kiasi, heshima iliyo ya wastani, uhuru wa kadiri na nguvu yenye mpaka ndio utawala wa haki. Mwenye uhuru wa kadri ni muungwana yeye mwenyewe na wengine, mwenye nguvu yenye mpaka hadhulumu wala hadhulumiwi. Mambo haya manne ni mbegu za mimea ya mazao ya hali njema, mapatano, usitawi na amani ya Dunia.

Shaaban Robert ametumia neno mimea kwani mimea hupandwa humea, hukua na kutoa matunda ambayo huvunwa. Hivyo ukipanda mmea ulio bora na ukasimamia makuzi bora ni lazima utavuna kilicho bora. Kiongozi bora huandaliwa katika misingi ya maadili mema. Dhihaka zinazotumika mfano katika sura ya nane kuwa mjumbe kutoka ardhi alikuwa kama mama anayemwandalia mahitaji mtoto ambaye bado hajazaliwa. Msemu huu unalenga katika kudidimiza vipawa vya watu jasiri wanaojitokeza hasa katika utawala au uongozi. Lengo ni kuziba nafasi na ubunifu wa chipukizi hususani katika nyanja ya uongozi.

Msemu maalumu kuwa Ngo'mbe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa ina tafsiri pana katika fasihi ya Lugha, kwamba kila mwenye asili haachi asili yake pia mcheza kwao hutunzwa. Kila unapopata tatizo lolote kimbilio la kwanza ni ndugu zako ili usaidiwe.

Riwaya ya kusadikika imeonesha jinsi wajumbe mbalimbali waliojitokeza na kwenda nchi za mbali kujifunza yaliyo mema, pamoja na shiida na vikwazo walivyopata wajumbe hao walirudi katika nchi yao ya Kusadikika ili kuleta mapinduzi kifikra na maendeleo kwa ujumla.

Nchi walizokwenda kutafuta elimu na fikra mpya ni mfano wa zizi. Matatizo magumu, mateso, na kero ambazo wajumbe walipata katika nchi za mbali ndiyo majeraha wao, wakisimama badala ya ng'mbe. Zizi lao ni nchi ya kusadikika. Dhima ya ufutuhi katika riwaya ya Kusadikika imelenga zaidi katika kuonesha aina mbalimbali za uongozi na utawala ulio bora ambao unatumia busara na kulinda haki za wananchi wake. Ndiyo sababu Karama katika sura ya tisa ameachiliwa huru kwamba hakuwa na hatia lakini maamuzi hayo yametokana na usimamizi bora wa sheria na ushirikiano wa vyombo vya dola vilivyo na uwezo wa kusikiliza na kupima uzito na dhamira za Walengwa kama ulivyokuwa kwa Karama.

Karama ni kielelezo cha mwananchi shujaa, mzalendo, mpenda haki na mwadilifu anayetetea maslahi ya wananchi wake. Watuhumiwa wote sita ambao ni Buruhani, Fadhili, Kabuli, Aumi, Ridhaa na Amini ni kielelezo cha mashujaa wachache wanaoweza kujitoka kwa ajili ya wengi na mfano wa kuigwa, Mfalme wa Kusadikika ameanesha umahili na ukomavu wa kiutawala katika kushirikisha wazee wa mahakama na hatimaye kutoa hukumu ambayo imewatendea haki watuhumiwa wote. Walibainika kuwa wao ndiyo wapiganaji halali na watetezi wa nchi ya kusadikika walio kandamizwa na uongozi wa sheria ya kimabavu.

Dhima ya ufutuhi katika riwaya hii ya Kusadikika inatuelekeza kuona umuhimu wa utawala wa pamoja hasa pale ambapo mfalme wa Kusadikika anaposhirikisha madiwani kucheua utetezi wa watuhumiwa na hatimaye kuafikiana na maamuzi ya kuwaachia huru watuhumiwa wote ambao ni watetezi wa kweli wa nchi yao ya Kusadikika.

1. Dhana ya Ufutuhi

Zipo fasili nyingi za neno ufutuhi, aghalabu nyingi ya fasili hizo zinalingana katika ufafanuzi mfano, “Ufutuhi ni mbinu ambayo mtunzi hutumia maneno au hali nyingine yoyote inayoweza kusababisha hadhira yake kupata furaha, kicheko/ucheshi. Kazi ya fasihi. Ufutuhi ni aina mojawapo ya tamthiliya ambayo huwa na maneno pamoja na matukio au matendo ya kufurahisha au kuchekesha ambavyo aghalabu hubebwa na tamathali za usemi. Ni uigizaji, mchezo, tukio la kuvutia tendo au maelezo yoyote yasiyo ya kawaida yenye lengo la kuvuta hisia au usikivu wa hadhira na kuwafanya wacheke au watabasamu.

Kwa mujibu wa OALD (2007), Futuhi ni uigizaji au mchezo, tukio la kuvutia, tendo au maelezo yoyote yasio ya kawaida yenye lengo la kuvutia hisia au usikivu wa watu na lenye kuwafanya watu wa cheke au tabasamu. Ufutuhi kupitia mbinu ya ubeuzi ukweli wake unauma na kuamsha hasira ingawa katika vichekesho ukweli hauuni sana. Ubeuzi unahitaji muda wa kufikiri ili kupata Dhana tarajiwa kupitia ufutuhi kwa mujibu wa ALD (2007) ufutuhi ni uigizaji au mchezo. Tendo au maelezo yoyote yasiyo ya kawaida yenye lengo la kutia hisia au usikivu wa watu na mazungmzo yenye kufanywa watu wacheke au watabasamu.

Wamatila (2007) anaeleza Dhana ya ufutuhi kuwa ni aina mojawapo ya tamthilia ambayo ina maneno pamoja na matukio au matendo ya kufurahisha au kuchekesha kwa mtizamo na maelezo ya wanazuoni hao, tunaweza kusema kuwa ufutuhi ni hali iliyojengwa na maneno, matukio au mazingira yoyote yenye mvuto au yasiyo ya kawaida yenye kuwafanya watu watabasamu au wacheke na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira husika.

Hivyo ufutuhi ni sanaa ya Lugha iliyoandaliwa kitaalamu kwa madhumuni, maalum ya kufikisha, ujumbe ulioandaliwa kwa jamii au hadhira husika. Ili kukidhi lengo la ufutuhi ni lazima vipengele vifuatavyo vizingatiwe. Kwanza Dhana na dhamira ziwe fiche katika fani. Watumizi wengi wa vitabu vya Kiswahili wamekuwa na mfumo wazi au kutoa ujumbe wa moja kwa moja ambao haufichiki. Lakini kazi nyingi za Shaaban Robert huwa zinaacha maswali mengi kwa wasomaji hasa pale ambapo ujumbe unafichwa.

Hivyo mimi nikiwa mtafiti nimezama kwa undani na kwenda kuchunguza ni kwa nini shaaban Robert katumia ufutuhi katika kazi zake?" Pili Mazingira, umri wa walengwa(kundirika) Kiwango cha Elimu,Lugha ya mawasiliano muda na vionjo vya hadhira vizingatiwe, Kwa ujumla ufutuhi ni njia ya kufikisha ujumbe kwa haraka, kwa gharama nafuu na unaamsha ari na utafiti katika kupata maudhui ya ujumbe ulio kusudiwa.

2. Kauli ya Tatizo

Riwaya nyingi za Shaaban Robert kwa msomaji wa kawaida huwa ni vigumu kubainisha maudhui au Dhana ya kazi husika ambapoinahitaji umakinifu, utulivu na upekuzi hata kwa mfano katika kitabu cha Kufikirika katika ukurasa wa 18 tunaona kuwa mtabiri amefanikiwa katika utabiri wake kwamba Mfalme na Malkia watapata mtoto. Kweli amezaliwa mtoto mume. Limetungwa shairi lenye beti nne nanukuu ubeti wa pili:

Jina lake milele

Lazima likumbukwe

Kama watu wateule

Na yeye anakiliwe

Nchi ijae tele

Mfano wa yeye

Daima kwenda mbele

Mambo yatazamiwe

Katika utenzi huu hususani ubeti huu wa pili mtunzi anasisitiza umuhimu wa kuandika kumbukumbu na kuweka Historia kwa faida ya vizazi vijavyo, pia anasisitiza juu ya uzazi kwamba familia wanapaswa kuzaa watoto wengi tena kwa aina ya mwanawe Mfalme yaani wanaume kwa lengo la kuongeza idadi ya watu na kuimarisha ngome ya utawala (ufalme). Katika Riwaya ya Kusadikika katika ukurasa wa namba ya kirumi vii, mtunzi Shaaban Robert ameandika sentensi yenye maneno machache lakini yamebeba maudhui ya kitabu chote cha kusadikika, nanukuu.

“Ngombe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa” Yaliyojitokeza kuanzia sura ya kwanza hadi ya tisa ya kitabu cha Kusadika yote yamelenga usemi huo. Mfano wajumbe wote kutoka nchi yao ya Kusadikika waliokwenda Kaskazini, Mshariki, Kusini, Magharibi, Mbinguni, na Ardhi wote walikuwa ni wa kujitolea kwa lengo la kuleta ukombozi wa kisheria na maendeleo katika nchi yao na mateso yote magumu waliyopata safarini walivumilia hadi wakarudi nchini mwao ingawa waliishia kushtakiwa wengine kufungwa lakini hitima yake wote waliokolewa na kuachiliwa huru chini ya utawala wa Mfalme wa Kusadikika baada ya kuona kuwa hawakuwa na hatia.

Mfano, Katika Riwaya ya Kusadikika ukurasa wa 50 aya ya tatu Mfalme wakati wa hukumu alinena hivi, “Naafikiana na ninyi (Madiwani) kabisa. Hapana hukumu nyingine iliyowezekana juu ya ushahidi uliokuwa mbele yetu. Zaidi ya hao natoa amri kuwa watu sita waliotajwa katika kesi hii, Burudani, Fadhili, Kabuli, Auni, Ridhaa na Amini wafunguliwe mara moja. Inasikitisha sana kuwa dhuluma juu ya watu hawa hazikuondolewa mpaka leo. Gerezani makao ya wahalifu. Watu hawa siyo wahalifu ila wafadhili bora. Wanastahili uhuru na heshima kubwa. Hasara zao lazima zifidiwe. Kusadikika inamshukuru sana Karama kwa kuhitimu wajibu wake”, hivyo baada ya miaka michache kupita mazungumzo yote yaliyoletwa Kusadikika na wajumbe wake yaliamsha bidii zilizokuwa zimelala. Matokeo haya chanya yanabeba ujumbe huo wa ng’ombe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa. Ambapo ufutuhi umetumika kufikisha ujembe.

1.5 Nia Kuu ya Utafiti

Kazi hii ya utafiti imetafiti kwa kina, Dhima ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert katika kuimarisha taalima ya uandishi na matumizi bora ya Lugha Ya Kiswahili.

1.6 Madhumuni Maalumu ya Utafiti

- (i) Kubaini matukio ya kifutuhi yanayojitokeza kwenye riwaya za Shaaban Robert na kama yana Dhana yoyote kwa jamii.
- (ii) Kuchambua na kuanisha miktadha mbalimbali ambayo Shaaban Robert ametumia na kujitokeza kama matukio ya kifutuhi katika riwaya zake.
- (iii) Kuanisha na kubaini athari zinazoweza kusababishwa na dhima nzima ya matumizi ya ufutuhi katika riwaya za Shaaban Robert.

1.7 Maswali ya msingi ya utafiti

- (i) Je kuna matukio ya kifutuhi yanayojitokeza kwenye Riwaya za Shaaban Robert na yana Dhana yoyote?
- (ii) Ni katika muktadha/miktadha gani Shaaban Robert ametumia matukio ya kifutuhi katika Riwaya zake?
- (iii) Je ni athari gani zinaweza kusababishwa na matumizi ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert.

1.8 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika maeneo yafuatayo

- (i) Kuchunguza Dhima Ya Ufutuhi Katika Riwaya Za Shaaban Robert Lengo Likiwa Ni Kuzibainisha Kuzitambua Na Kuzichambua Baadhi Ya Kazi Za Shaaban Robert Ili Kuhimiza Matumizi Ya Ufutuhi Katika Uandishi Na Uwasilishaji Wa Kazi Mbalimbali Za Uandishi.
- (ii) Kuamsha Ari Kwa Watunzi Na Waandishi Chipukizi Wa Kuandika Vitabu Kwa Kufuata Mfumo Wa Mtaalamu Mkongwe Wa Kiswahili Ambaye Pia Ni Gwiji La Kiswahili Shaaban Robert.
- (iii) Kuhamasisha Jamii Asilia Alikoishi Shaaban Robert Kujitambua Kuwa Wao Ni Sehemu Muhimu Ya Historia Ya Kiswahili Na Kwamba Wanatakiwa Kuyaenzi Maeneo Ya Kihistoria Alikofanyia Kazi Na Hata Alikozikwa Shaaban Robert Kwa Faida Yetu Sote Na Vizazi Vijavyo. Kwani Baadhi Ya Tungo Zake Zenye Ufutuhi Mkubwa Zimetokana Na Lugha Yake Asilia Mfano: Kiyao, Kidigo, Kibondei Na Kizigua.

- (iv) Kuwahimiza Watafiti Kubuni Mbinu Bora Za Kufundishia Somo La Kiswahili Na Kutumia Uwanja Wa Kiswahili Kuunganisha Vijana Ambao Huunda Vikundi Vya Sanaa Na Kuondoa Tatizo La Ajira Kwa Vijana. Mfano Kikundi Cha Futuhi Kilichoko Mwanza Na Komedi Halisi Ya Dar es Salaam Hawa Ni Ashirio Kwamba Jamii Inaweza Kuelimishwa Kupitia Uwanja Wa Maigizo Yaliyosheheni Ufundi Na Mbinu Bora Za Kifutuhi Katika Kuwasilisha Ujumbe Na Kuelimisha Jamii.
- (v) Kuhimiza Uandishi Wa Vitabu Unaomfanya Msomaji Kujiuliza Maswali Mengi Ili Kuibua Moyo Na Ari Ya Kujifunza Na Ubunifu Wa Lugha Iliyo Fiche. Dhana Inatakiwa Iwe Na Ubunifu Ili Kuleta Hali Ya Ushirikishwaji Kati Ya Mtunzi Wa Vitabu Na Msomaji. Mfano Katika Riwaya Za Kusadikika, Kufikirika, Siku Ya Watunzi Wote Na Adili Na Nduguze Hivi Ni Vitabu Vya Mfano Wa Kuigwa Kutokana Na Utunzi Mahiri Wa Shaaban Robert Na Vimelenga Kupanua Matumizi Ya Dhima Ya Ufutuhi Katika Kufundisha Na Kuelimisha Jamii.

1.8.1 Matokeo ya Utafiti

- (i) Nimebaini jinsi ya kuwasaidia watu wengi hususani watunzi na waandishi wa vitabu, wanafunzi wa ngazi zote, waalimu, wakufunzi, wakuza mitaala, watunzi wa sera za Elimu nchini na wapenzi wote wa lugha ya kiswahili. Mtaala wa lugha ya Kiswahili utilia mkazo matumizi ya vitabu vya Shaaban Robert.
- (ii) Kuandika vizuri na kusoma tasnifu (na baadaye vitabu) itakayotokana na utafiti huu ili kupata ari ya kuzisoma kazi za Shaaban Robet na kuyaelewa

vizuri zaidi maudhui yaliyomo katika maandishi hayo hususani yeye maudhui ya ufutuhi.

- (iii) Nimeambua na kubaini mchango wa Shaaban Robert katika kuimarisha na kuendeleza utamaduni wa Kiswahili hivyo nashauri jamii kuiga mitindo yake ya maandishi na uandishi wa vitabu.
- (iv) Nimebaini na kuzifahamu sheria za utunzi na uandishi wa vitabu, pamoja na miktadha mbalimbali aliyokutana nayo Shaaban Robert wakati wa maisha na uhai wake. Hivyo elimu hiyo nitairithisha kwa jamii kwa kupitia machapishi mbalimbali
- (v) Nimeelimika jinsi ya kuhamasisha walimu, wanafunzi, wanafasihi, pamoja na wasomaji wengine kwa ujumla, kupenda kuzisoma na kuzihakiki kazi za Shaaban, kama alivyoathirika prof. Sengo ambaye anadai hadi leo kuwa Shaaban Robert ndiye mwalimu wake mkuu wa Kiswahili na uandishi wake umemfikisha kwenye kiwango alichonacho sasa.
- (vi) Nimewezeshwa kuchambua matukio ya kifutuhi yaliyomo katika Riwaya za Shaaban Robert. Pia nitawahamasisha watafiti kufanya tafiti nyingi katika Riwaya za Shaaban Robert na wengineo ili kubainisha vikwazo vilivyowakabili watafiti waliotangulia na jinsi ya kutatua.
- (vii) Nimebaini umuhimu wa kuwashawishi waandaaji sera ya elimu nchini katika kuzingatia masuala ya utunzi wa vitabu uhifadhi na jinsi ya kurithisha Elimu kwa vizazi vijavyo.
- (viii) Nimeelimika juu ya matumizi ya runinga na redio kama vyombo vya kufundishia na kuelimisha jamii juu ya matumizi ya ufutuhi kama njia ya

kupashana habari na kuimarisha maadili mema na burudani kwa ujumla mfano

- Vikundi vya sanaa kama kaole, TOT plus
- Vikundi vya sanaa na uchekekeshaji mfano komedi orijino ya Dar es salaam, mzee Majuto

1.9 Eneo la Utafiti

1.9.1 Eneo

Eneo husika ni mikoa ya Dodoma, Tanga na Dar es-Saalam.

1.9.2 Mipaka ya Utafiti

Mipaka ya utafiti ni shule kongwe za sekondari zilizoko Manispaa ya Dodoma hususani wanaosoma somo la Kiswahili, wazee mashuhuri walioishi na Shaaban Robert huko Mpwampwa, Dodoma akiwa bado ni mtumishi wa serikali. Pili Dar es Salaam kwenye vyanzo vya maktaba mbalimbali zenye kazi za uhakiki za Shabaan Robert. Ufukweni Kigamboni ndipo alipozaliwa babake Ufukwe bin Suleiman ambaye alikuwa mtumishi wa Bw.Robert.Kwa mapenzi ya Bwana Mkubwa huyo Ufukwe aliitwa Robert.

Tanga na viunga vyake ambapo imekuwa rahisi kuwapata ndugu, jamaa na marafiki wa Shaaban Robert. Vijiji vilivyotembelewa ni Machui alikozaliwa na kukulia, Vibambani alikozikwa. (Handeni) nyumbani kwa marehemu Yusufu Ulenge ambaye alikuwa Mnuna na kipenzi cha Shaaban Robert. Pia mtafiti ametembelea jengo la makumbusho lililoko Tanga mjini na huko vibambani. Utafiti pia umejikita katika

Riwaya nne za Shaaban Robert ambazo ni Kufikirika (1946), Kusadikika (1948). Adili na Nduguze (1951) na Siku ya Watenzi Wote (1961).

1.9.3 Ukubwa wa Uteuzi

Nimeweza kuwafikia watu wapatao 320 idadi iliyolingana na maandalizi tangu awali.

1.9.4 Uteuzi wa Walengwa

Kwa vile kazi hii imetafiti dhima ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert walengwa wakubwa ni walimu, wanafunzi walioko sekondari na vyuo vya juu lakini pia nilishirikisha viongozi mbalimbali wa vijiji na taasisi za umma mfano Mpwampwa, Wakurugenzi wa mkoa wa Chuo Kikuu huria cha Tanzania vijana, wasichana wa miaka 18 na kuendelea na viongozi wa dini wakiwemo mashehe, wachungaji na mapadre.

1.9.5 Upatikanaji wa Uteuzi

Uteuzi huu nimeupanga katika makundi matano ni wanafunzi wa sekondari, vyuo vya elimu ya juu, wafanyakazi, watu wa zima na viongozi wa dini na taasisi mbalimbali mbinu hii imetumika kutokana na sababu za rika, kijiografia, utaalumu na mahusiano kati ya wateuliwa na Shaaban Robert. Angalia jedwali namba 1.1.

Jedwali Na. 1.1: Kuonesha Upatikanaji wa Uteuzi

Lengo La Jumla-Watafitiwa	Wanafunzi Sekondari	Vyuo Vya Juu	Wafanyakazi	Watu Wazima	Viongozi Wa Dini/Taasisi
320	100	130	40	30	20

Chanzo: Utafiti wa Mwaka, (2010)

Jedwali Na. 1.2: Kuonesha Makundi ya Uteuzi Kijinsi

Lengo Jumla Kuu ya Watafitiwa	Wanafunzi Sekondari				Wanavyuo Elimu ya Juu				Wafanyakazi				Watu Wazima Wasio Watumishi				Viongozi wa Dini na Taasisi			
	ME	KE	JUMLA	%	ME	KE	JUMLA	%	ME	KE	JUMLA	%	ME	KE	JUMLA	%	ME	KE	JUMLA	%
320	50	50	100	31	80	80	130	40.62	20	20	40	12.5	20	10	30	9.4	10	10	20	6.25

Chanzo: Utafiti wa Mwaka, (2010)

1.9.6 Makundi ya Uteuzi Kijinsi

1.9.7 Eneo Lililoongezwa

Kutokana na walengwa kutawanyika katika maeneo mbalimbali nimelazimika kuongeza eneo la ubungo Dar es salaam ambako mtoto wa marehemu Shaaban Robert aitwaye Ikkal anakofanyia kazi. Mtafitiwa alipatikana na alitoa ushirikiano mzuri wakati wote wa utafiti.

1.9.8 Sababu za Kufanya Utafiti Katika Eneo Hili

- (i) Utafiti unalenga kuchambua Dhima ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert hivyo ni lazima watafiti wawe ni wale wanaosoma/waliosoma riwaya za Shaaban Robert au wanaofundisha.
- (ii) Lakini pia ili uweze kujua chimbuko la kazi za Shaaban Robert au wanaofundisha kazi za Shaaban Robert ni lazima ujue maisha yake na kazi nyinginezo alizofanya. Taarifa hizi utazipata kupitia maandiko, Nyumba za Makumbusho na kupitia nduguze jamaa na marafiki. Mfano jumba la Makumbusho Tanga, kituo cha utamaduni kijijini Machui Tanga.

1.9.9 Matatizo Vikwazo / Utatuzi

Matatizo/ Vikwazo

- (i) Gharama kubwa za utafiti
- (ii) Kutumia muda mwingi na kutafuta walengwa mara kadhaa.
- (iii) kutopatikana watafitiwa kwa wakati muafaka na wengine kukataa kutoa ushirikiano.

- (iv) Elimu duni na dhana potofu ya jamii dhidi ya watafiti.
- (v) Hali mbaya ya hewa mfano mvua, miundo mbinu duni.

1.10 Utatuzi

- (i) Nilifanikiwa kutafuta fedha za ziada (Mkopo)
- (ii) Nilitumia njia shirikishi mfano viongozi/ watu maarufu kuwafikia watafitiwa
- (iii) Niliimarisha uhusiano bora ndani ya jamii.
- (iv) Nilitembelea eneo la utafiti kutegemea na hali ya hewa inapokuwa nzuri.

SURA YA PILI

2.0 MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Nadharia imefasiliwa na wataalamu kuwa ni kauli za kisayansi zinazotokana na matokeo ya muda mrefu ya tafiti juu ya tatizo moja hilo. Wataalamu wengi mfano; Massamba (2004), Owhida (2006), Sengo (2009) wameeleza Dhana ya nadharia kama ilivyofasiliwa hapo juu. Nadharia yeweza kuwa mawazo ya mtu mmoja au kundi la watu kuhusu jambo au kitu ambacho kinaweza kuwa cha ukweli au cha dhahania/kubuni, aghalabu kinaweza kuwa na mwekeo wa watu, jamii, kundi la watu au mtu mmoja na kusaidia kupata ukweli au hata kuthibitisha ukweli awa jambo kwa lengo maalumu lilokusudiwa (Owhida, 2006).

Sengo (2009) anasema nadharia ni wazo kuu, fikra kuu, mwongozo mkuu na mtu au watu (jamii), wa pahala Fulani, wakati Fulani, kwa sababu Fulani. Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kufasili jambo.

2.2 Nadharia Mbalimbali

2.2.1 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na nadharia ya umaana. Umaana ni taaluma inayoshughulikia na kufasir/kufasili matini kwa kuzingatia maana. Hivyo kiini cha nadharia hii, ni kuzingatia maana ya matini. Chimbuko la nadharia hii ni katika uchambuzi wa falsafa katika matini za kidini, hususani dini ya kikristo. Msingi mkubwa wa nadharia ya umaana ni imani ya kwamba matendo ya binadamu

yanaathiriwa kwa njia mbali mbali na asasi tafauti zilizoko katika mazingira yake. Kulingana na nadharia hii ya umaana, uelewaji wa maana kwa wasomaji, huhusisha kuyajua mambo mbalimbali yaliyomzunguka mtunzi, wakati au kabla ya kuitunga kazi. Ni vigumu mtunzi, iwapo msomaji au mhakiki hatahusisha mambo hayo. Newton (1997), amefafanua kuwa dhima ya msingi ya uhakiki wa matini kwa msingi wa umaana ni kuhusisha muktadha asili uliomzunguka mtunzi na utunzi wenyewe. Uhusishaji huu husaidia kubaini tafauti iliyopo kati ya maana ya matini na umuhimu wake. Hivyo, nadharia ya umaana, hujikita zaidi katika kuibua dhamira asili ya mtunzi kwa kutumia ithibati zozote zipatikanazo katika kazi hiyo.

Madai ya msingi ya nadharia ya umaana yanahusisha Dhana mbali mbali kama vile duara la kimaana, utukuzaji pamoja na ile ya uhuishaji wa sarufi, kisaikolojia na kimuktadha. (Senkoro, 1987, Wamatila, 2002, Genhald, 1964, Eaglton, 1996). Katika suala la duara la kimaana, Senkoro (1987:9) anaeleza kuwa, katika usomaji kuna mviringo wa kiamaana ambao humfanya msomaji aende mbele na nyuma, kushoto na kulia, mwa yale yaongelewayo katika kazi ya fasihi. Hadhira huwa inabashiri na kuhusisha (mambo) yanayopitiwa maishani mwa washiriki hao.

Dhana ya utukuzaji katika nadharia ya umaana ina maana ya jumla ya makisio mbali mbali ambayo msomaji au mhakiki wa kazi ya fasihi huwa nayo punde aishikapo kazi yoyote ya kifasihi. Hii ni hatua muhimu ya kuanzia katika kuelekea kwenye upatikanaji wa maana. Pamoja na kufanya makisio hayo, msomaji hupaswa pia kuihuisha miktadha mbali mbali ya utunzi wa kazi. Wamatila (2002:193), anafafanua kuwa Dhana ya uhuishaji hususa ni ule wa saikolojia, aliasisiwa na Dilthy (1983-

1911). Alisisitiza kuwa kuna umuhimu mkubwa wa mhakiki au msomaji kuufufua muktadha asilia wa kazi inayohusika na kujaribu kujiweka katika muktadha huo ili aweze kuipata maana halisia ya matini. Kwa mujibu wa mawazo yake, kazi mbali mbali za kifasihi zinaweza kuwa na maana mbali mbali kwa wasomaji mbali mbali. Aidha, Dhana ya uhuishaji inasisitiza kuwa ili kuelewa na kusiri maana ya matini, lazima msomaji au mhakiki azame katika kuuelewa mtindo wa maneno na sentensi zilizotumika katika matini.

Hivyo, nadharia ya umaana, itatumika kuchunguza matukio yakifutuhi katika kazi za kitutumbi za Shaaban Robert, kwa kuzingatia hatua zifuatazo, kurudia na kubaini maana yake kutokana na fikra binafsi za mtafiti kuhusiana na lugha na matukio mbali mbali yaliyojitikeza, kuhusisha vipengele vingine vya kimaisha kama vile matukio ya kihistoria yaliyojili kabla au wakati wa mtunzi. Kisha kuzisoma nadharia zake zilizobainishwa kutumiwa, kielezeo katika utafiti huu, ili kutafuta kuwako kwa mshikamano wa matukio hayo katika nathari hizo. Hatimaye. Hii itasaidia kupata maana, dhima na athari za matukio hayo.

2.2.2 Nadharia ya Mtu -Utu

Sengo (2009) anaelezea nadharia ya Mtu –Utu kwa Afrika na Mwafirika, Ustaarabu, hekima, busara, fikra, mawazo na hadhari za kimaisha kwa watu. Mtu ndiye khalifah, mlezi, mtunzi na mhifadhi wa yote anayotaka, anayoshiriki kuyaunda na yajayo usoni mwake leo au kesho. Ukarimu, takrima, wema bashasha, tabasamu, huruma, usafi, kazi kuwahi, furaha, raha subira, ukweli, uaminifu, udugu wa kiukoo, yote hayo yamo katika sifa za mja. Upande wa pili wa shilingi ya mtu, unajulikana kuwa

upo lakini haukubaliki ila pale ambapo tunautumiya uhasi huo kwa kumharibiya mtu uchanya wake. Mtu- kwao. Ikisema Afrika, ndilo bara la mwafrika. Mengine yapo na watu wa huko, wana yao. Kimsingi utu unatakiwa uwe mmoja. Tafauti ni za kihulka kitabiya na kimazingira.

Nadharia hii inagusa mambo mbalimbali ya maisha ya kila siku ya mwanadamu. Mfano katika Riwaya ya Siku ya watenzi wote ukurasa wa 7 imeonesha jinsi mtu anavyokuwa mnyenyekevu na mwenye adabu anapokuwa na shida lakini akipata atakacho huweza kusema maneno au kushukuru au kusema maneno ya kifadhili mfano ndege akiwa katika kichaka kimojawapo usiku huimba kucha:

Kichaka hiki kizuri,
Kwa marashi na uturi,
Harufu yake si nzito
Kwa tamu na manukato

Kwa sababu humpa hifadhi ya usiku. Na asubuhi yake hugeuka akiimba kashifa kutwa

Kichaka hiki kichafu,
Kwa uvundo na harufu,
Ya guguno na kutuzi
Na ubaya wa punzi

Kwa sababu hana haja tena ya hifadhi. Nadharia ya Mtu- Utu kupitia Dhima ya ufutuhi katika Riwaya hii inadhihirika kuwa utu wa mtu ni utu.

2.2.3 Nadharia ya Dini na Mtu Binafsi

Uhusiano uliyoko kati ya Mtu (muumini) na kile kitovu cha dini yake, ambacho huyaongoza matendo na maisha yake, hatutaki ieleweke kuwa mwanadamu ni mtu asiyeweza kutengwa na jamii yake, Omari (1981). Dini humhusisha muumini na Mungu na Maisha ya baadaye. Ingefaa kuangalia jinsi imani hiyo inavyomwongoza kutenda matendo Fulani na siyo mengine. Kadharika, jinsi kiongozi wa dini anavyotazamwa na watu wa jamii na jinsi anavyoheshimu hadhi yake. Wazo hili la jinsi dini inavyoweza kumfanya muumini atende matendo yake kwa njia Fulani tafauti na yule asiye mfuasi wa dini, Nadharia hii ilianza kujadiliwa kinadharia miaka mingi iliyopita na wanafalsafa wengi.

Weber aliona kuwa ulikwepo uhusiano kati ya mafundisho ya Kikristo, kati ya wasio Waroma, hasa wale wa madhehebu ya Kikalvini, na uchumi uliyopo katika jamii. Aliona kuwa mafundisho ya maadili yaliyojengwa katika imani ya madhehebu hayo, yalisaidia kukuwa kwa ukabila. Imani ya Kikalvini, hukazia maana ya wito. Na kwa vile kila kazi haina budi kutazamwa kama wito wa Mungu, kila mmoja alitakiwa afanye kazi kwa bidii zaidi na zaidi. Nadharia hi ya Dini na Mtu binafsi ni muhimu katika mchango wa kazi hii, kwani inagusa moja ya kazi ya nyimbo pale ambapo husisitiza kufanya kazi.

Kwa hakika ni hatari kuitazama fani hii kwa macho ya dharau kwa kudanganywa na “wakubwa” kuwa fasihi-simulizi na utamaduni kwa jumla, hauna maana katika maendeleo ya nchi na jamii. Uzushi huu ni wa kiibilisi sawa na ule wa kusema bara la Afrika ni kiza kitupu.

2.2.4 Nadharia ya Fasihi na Jamii

Fasihi ni taasisi ya jamii na uhusiano wake na jamii hauwezi kupuuzwa. Mmoja wa wanao unga mkono Dhana hii ni Escarpit, R (1974) ambaye anasema;

“Fasihi lazima ichukuliwe kama iliyo na mahusiano usiotatanika na maisha ya jamii. [tarijama yetu].

Fasihi ni tasisi ya jamii kwani hutumia lugha (ambayo ni zao la jamii) kwamba fasihi ni sehemu ya maisha ya jamii. Maisha Kuhusu uhalisiya wa jamii, hata kwa mtu binafsi ni mambo ambayo Werele na Werren (1949) wanashadidia kwa kusema;

“Uhusiano kati ya fasihi na jamii hujadiliwa kwa kuanza na kauli alioitoa De Bonaid kwamba ‘fasihi ni kielezo cha jamii’ [tarijama yetu].

Kwa kupitia nadharia hii, moja ya kazi za fasihi ni kuhifadhi historia ya .Kwa kusema kazi za fasihi tunaweza kupata historia ya jamii hiyo. Mfano, vipindi maalumu vya mfumo wa maisha wa jamii. Morani (Mbogo, 1993) na Kivuli KInaishi (Mohamed, (1990) ni mifano ya kazi zinazoonesha historia ya unyonyaji, unyanyasaji, rushwa na uongozi mbaya kwa jamii ya Tanzania. Zote hizi ni mifumo ya jamii katika Nyanja za maisha, pamoja na mila na desturi zake Hivyo basi, mtafiti anaona kwamba kauli ya fasihi ina uhusiano mkubwa na jamii ni dhima yenye mshiko. Tunasema, ni muhimu kuichukulia fasihi kama zao la jamii ambalo nalo huathiriwa na jamii inatoa Nadharia hii pia inatoa mchango kwa kuonesha historia ya jamii hiyo. Ingawa si historia kuhusu jamii ndio kielezo cha mila na desturi.

2.2.5 Nadharia ya Uasilia

Nadharia ya uasilia, msingi wake mkuu ni kutoa picha ya maisha kama yalivyokuwa (Kwa Ukweli wote) na kuelezea maisha yalivyo sasa. Ntarangwi (2004); aliandika:

Katika karne ya kumi na tisa, mtaalamu wa elimu ya viumbe hai Charles Darwin, alishikilia kwamba binadamu alikuwa chini ya himaya ya maisha ya asili na kamwe hakuwa na roho (soul) wala uhusiano wowokate wa kidini uliyokiuka kaida za ulimwengu halisi. Hivyo basi binadamu alichukuliwa kama mnyama wa tabaka la juu ambaye tabia yake hutegemea uzawa wake na mazingira yake. Karne za hivi karibuni wanasayansi wa Ufaransa wameanza kukanusha vikali upuuzi wa Darwin.

Kwa msingi huo uasili ni chanzo cha maisha, hulka, mitazamo na mipangilio ya binadamu kama tuonavyo leo. Huu ni mtizamo unaochukulia maisha ya binadamu yanavyoanza na kiwango cha chini (cha kinyama) hadi cha juu (cha ustaarabu) Nyingi ya Hadithi na visa vingi vya asili kuhusu tamaduni zetu, vyaweza kuchunguzwa kwa kutumia mtizamo huu. Nadharia hii huangalia zaidi mwanzo wa binadamu na maendeleo yake yanayokuwa, haijiki sana kwenye mila na desturi za jamii hiyo.

Nadharia hii imegusa mwandishi Shaaban Robert kwani amekana kuheshimu uasili wa Mwafrika na Riwaya za Kusadikika, Kufikirika Siku ya Watenzi Wote, Adili na Nduguze zote zimeweka msisitizo na kutoa heshima na tuzo maalumu kwa uasili wa Mwafrika na harakati zote za ukombozi wa nchi zao.

2.2.6 Nadharia ya Ndani –Nje

“Uhalisia wa kiafrika” “Fasihi ina kwao”na “Ndani-Nje” ni nadharia na mbinu ndugu za kuitumikisha fasihi kwa manufaa ya jamii. Ndani, ni sirini mwa jamii. Mtu mgeni si rahisi kuzipata siri za jamii, ishara za watu ila kwa kukaribishwa, kuaminiwa na kuthaminiwa sana.”Asiyekujua hakuthamini, siri ya mtungi aijua kata,

ya kaburi aijuaye maiti na ugumu wa kusoma aujua msomaji". Nazi nzima huthibitika baada ya kuivunja. Nadharia hii (Sengo: 1985) ina manufaa makubwa katika kuakisi ukweli.

Nadharia hii ni muhimu sana katika kazi hii ya fasihi ya Lugha hususani matumizi ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert. Kama mtu hayupo ufutuhi haupo kama ufutuhi haupo sanaa ya lugha haijakamilika. Kama hadhira haipo ujumbe ulioandaliwa hautafikishwa kwa walengwa. Hivyo upo mfano wa kutegemeana. Katika Riwaya ya Adili na Nduguze mtunzi mkongwe wa lugha ya Kiswahili Sheikh Shaaban Robert ametumia ufutuhi na umahiri wake mkubwa umeonekana pale ambapo ametaja habari za Malaika, Majini, manyani na viumbe wa ajabu lakini vikiwa ni viwakilishi vya lengo kuu. Maudhui makubwa yaliyobebwa na Riwaya hii yanatilia mkazo juu ya ardhi na mimea yake, machimbo na hazina zake, mifugo na mazao yake, utajiri na Baraka zake, ahali na heshima zao, ndugu na matendo yao na utawala na mbinu za kutawala.

Mfalme Rai akiwa mfalme mwadilifu wa ughaibu na ambapo amefananishwa na rangi za pundamilia zilizogawanyika katika theluthi tatu ya kwanza Rai alikuwa msuluhifu, hivyo alipendwa na watu, ya pili kwa kuwa alipenda watu na wanyama aliheshimika kama mtunzaji mkuu wa wanyama. Theluthi ya tatu alikuwa na uwezo mkubwa kiutawala hivyo alifananishwa na Daudi.

Riwaya hii ya Adili na Nduguze kuanzia sura ya kwanza inayomfafanua mfalme Rai, pia imetaja msukosuko inayompata mwanadamu katika maisha yake na jinsi ya kupambana nayo. Mfano katika sura ya nne hadi ya saba mtunzi amepambana

bayana juu ya utafutaji mali, jinsi ya kutunza fedha na kumbukumbu lakini ameonesha athari za kutapanya mali kwa matumizi ya anasa inayoweza kumfilisi mtu. Ufutuhi umejitokeza wazi katika sura ya tatu mtunzi anaposema Tafakuri ilimwonyesha Adili kuwa ukali wa mbwa hutokana na msasi, Mbwa wa msasi mkali ni wakali pia. Ana maana kuwa mtoto wa nyoka ni nyoka au mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

Sura ya nne inataja majina ya ndugu zake Adili yaani Hasidi na mwivu. Athari za kuita majina yenye visa inaathiri tabia ya mtu kama ambavyo hao waligeuzwa kuwa manyani baada ya kumtendea maovu ndugu yao Adili kwa kumtosa baharini ingawa badae aliokolewa. Anasema Adili na nduguze walilelewa mpaka wakawa watu wazima wenye vichwa vinanyofunzwa lakini mioyo iliyosahauliwa, Busara kubwa kichwani haina faida kama moyoni hamna chembe ya wema.

Katika sura ya tano mwandishi ametumia ufutuhi katika kueleza uadui, uvivu, ulevi na anasa ni adui wakubwa wa maendeleo. Mshawasha wenyewe ukitokana na mtu unayempenda au tamaa ya utajiri. Sura nzima inaeleza athari za tamaa, wivu hila na husda za binadamu. Adili ameonesha moyo wa huruma na wema kwa kumwokoia Indu ambaye uligeuka kuwa mwanadamu aliyemsaida babaye mafunzo ya kiufutuhi ni kwamba usimdharau usiyemjua na wema siku zote una malipo makubwa, kama jinsi nyoka aliyeteketezwa kwa moto na kuwa majivu jinsi alivyogeuka kuwa kijito chenye maji mengi na mazuri yaliyowaokoa msafara wa Adili merikeburi kutokana na hatari ya kiu. Katika sura ya saba na nane matumizi makubwa ya ufutuhi yanatupa ujumbe wa jumla kuwa ujasiri na uvumilivu kuwa ni silaha kubwa katika kuleta maendeleo. Adili alitembelea mji wa mawe akapitia hali nyingi na kupata vitu vya

thamani pia alifanikiwa kukutana na msichana mzuri ambaye kumbe ndiye aliyewahi kumwookoa kutoka kwa tandu aliyedhamiria kumtekeleza. Ingawa msichana huyu inaonekana kuwa ni jini lakini ujumbe wa kifutuhi uko palepale kuwa tenda wema nenda zako usingoje shukrani kwani ipo siku utalipwa na mwenyezi Mungu. Kama usemi wa binti mfalme ulivyomwonyesha Adili kuwa, “Turufu huenda kwa mchezaji siku zote” Laiti Adili asingelikwenda safari na kuwaacha wenziwe waliyoogopa na akatafuta tafuta asingalikutana na bahati ile ambayo hakutazamia kuja katika ndoto zake yaani kupata mali, vito na makomamanga yaliyowashibisha abiria wenzake ndani ya melikabu.

Kutoswa kwa Adili baharini na ndugeze hadi kuokolewa na binti aitwaye Huria ambaye ni jini inaonesha matunda ya kutenda wema ingawa katika sura ya kumi na moja shaban Robert amefafanua juu ya vikwanzo anavyopambana navyo msichana katika makuzi yake jinsi mvulana Hunde mwenye sura mbaya alivyomtamani Huria. Shabani Robart anasema wanawake hukutana na mikasa mingi mibaya duniani mioyo yao hulemewa na haja zilizokubalika masikio yao hutiwa uziwi kwa maombi ya haraka na miili yao ni mawindo ya jeuri daima, wanaume wana inda mbaya na ufnisadi unapowapofusha. Wema wa Adili uliingiwa na dosari ya huzuni alipolazimika kuyaadhibu manyani ambayo alijua fika kuwa ni nduguze waliogezwa kuwa manyani hivyo kama adhabu kutokana kwa hila zao. Kwa huruma yake kila mara baada ya kuyapiga manyani aliyanasili akilia kwa utenzi huu:

Nala sumu ndugu zangu, msabe naona tamu,

Takatifu kubwa kwangu, kuadhibu Roho yangu damu,

Sina raha ndugu zangu, neno hili kwagu gumu.

Shabaan ametumia ufutuhi wa hali ya juu sana ili kutoa ujumbe kuwa tendo baya lolote ni vigumu kumtendea nduguyo hata kama umelazimishwa. Lakini dhamira za watendewa hubakiwa na simanzi kuu hata kama ni wakosaji kama walivyokuwa wale manyani, Ujasiri wa Adili kula pamoja na manyani na kulala nao chumba kimoja ni kielelezo cha upendo na ujasiri wake bila kujali kauli na minong'ono ya watu dhidi yake. Manyani yaliposamehewa makosa yao na mfalme wa majini hadi wakarudia utu wao.

Shaaban Robert anaonesha uwezo mkubwa alionao binadamu. Anasema mwanadamu alikuwa bora kuliko jini. Majini kokote iwe katika jua, Mwezi, Mushtara, Zebaki, Zuhura, Mirithi, Sumbula Zohari Sarateni, Kausi na utaridi hayakuweza kushindaana na watu katika Ardhi. Majini yaliweza kugeuza watu katika umbo lolote, lakini watu waliweza kufunga majini yote katika chupa moja na magereza yao yalikuwa mabaya sana. Kama mtu asingalikuwa mzembe mwenyewe, busara ya jini ingalikuwa busara yake. Alipaswa kuheshimiwa kama ataridhia heshima yake.

Shaaban Robert ameonesha uwezo mkubwa alionao mwanadamu aliopewa na mwenyezi Mungu kuwa ni mtawala wa vitu vyote vya Dunia hii vikiwemo viumbe hai, uoto wa asili, maji, hata majini, lakini anatumkumbusha kuwa daima inafaa kutubu pale unapokosea kama ambavyo manyani walivyosamehewa baada ya kutubu na kurudishwa kuwa wanadamu na jinsi walivyo mshukuru Mfalme na wakaahidi kuwa walikoma kutenda dhara kwa ndugu yao, na kwa kitu chochote kilichokuwa ndani ya Mazingira yao.

2.3 Nadharia Tete

Nadharia tete inafafanuliwa na vipengele vikuu vitatu ambavyo pia vinategemeana. Kwanza yapo mambo ambayo hayategemei jambo jingine katika mabadiliko. Haya yanaitwa Vigezo vinavyojitegemea ambavyo ni Elimu, Mila, desturi na Mazingira. Pili ni yale mambo ambayo yanaweza kubadilika kutokana na hali ya kipindi hicho yanayoitwa “Vikwazo” ambavyo vinajumlisha Sera za Nchi, utamaduni, hali ya uchumi na Muda.

Tatu hili ni zao la mwisho ambalo ni “Matokeo” ambayo kwa utafiti huu unatoa mbinu bora za kubaini Dhima ya ufutuhi hususani katika Riwaya za Shaaban Robert. Mfano, maadili husababishwa na vikwazo kama vile Sera za nchi, utamaduni, hali ya uchumi, na muda au mihula, Ni dhahiri kuwa katika utekelezaji wa elimu wa mazingira ni lazima yaingiliane na utamaduni kazi hii ya utafiti imeangalia pia maadili mema ya jamii alioishi marehemu Shaaban Robert.

Baadhi ya watunzi wa vitabu wamekuwa hawazingatii maadili ya kitanzania. Hivyo kwa taswira hii una nadharia tete zifuatazo:

- (i) Kuwepo na mwendelezo wa fasihi Simulizi kuendeleza na kulinda kazi za Shaaban Robert
- (ii) Sera ya nchi juu ya uchapishaji vitabu, utamaduni hali ya uchumi na mabadiliko ya kifikra ndani ya jamii ni kikwazo katika upatikanaji wa wasomaji vitabu vya Shaaban Robert.
- (iii) Kutokuwepo na shughuli au matukio ya kiushindani miongoni wa watumiaji na waandishi wa vitabu vya Kiswahili yanayolenga matumizi ya ufutuhi katika

kusoma kutunga na kuchambua vitabu vikiwemo vya Shaaban Robert ni kikwazo kikubwa.

Kutokana na nadharia tete zilizojitokeza hapo juu nimechimbua vikwazo vyote na kubaini umuhimu wa nadharia hii ambao ndio kiini cha utafiti wa Dhima ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert.

2.4 Nadharia Kiongozi

Uchambuzi wa nadharia mbalimbali na mwelekeo wa nadharia tete, vinamfanya mtafiti apate baadhi ya nadharia zitakazo mwongonza. Lakini hakuna nadharia inayojitosheleza katika kazi za fasihi. Aghalabu, mtafiti huweza kutumia nadharia zile ambazo humsaidia ili kuweza kuthibitisha wazo lake. Katika kazi hii nadharia tatu zimetumika kutuongoza, ambazo ni Nadharia ya Utu wa mwanadamu na Fasihi, Nadharia ya Fasihi na jamii na Nadharia ya Chimbuko la Fasihi.

Mtafiti anapofanya uchambuzi wa Nadharia Mbalimbali kwa kuhusisha na Nadharia tete hatimaye hupata Nadharia Kiongozi ambayo ndiyo mwongozo wa Nadharia zote alizozichambua. Kazi kuu ya mtafiti ni kuchambua Nadharia zenye uhusiano na mada aliyoitaua kwa lengo la kuweza kuthibitisha wazo lake.

Katika Kazi hii Nadharia sita zimeteuliwa na kutumika kutuongoza nazo ni Nadharia ya utafiti. Nadharia ya mtu - utu, Nadharia ya Dini na Nadharia ya mtu Binafsi, Nadharia ya Fasihi na Jamii, Nadharia ya ndani nje, Nadharia hizi zote zimefafanuliwa na kuonesha umuhimu na uhusiano mkubwa na mada kuu iliyoteuliwa na mtafiti ya Dhima ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert,

uchambuzi wa Nadharia mbalimbali na mwelekeo wa Nadharia tete zinamwelekeza mtafiti kupata nadharia zitakazo mwongoza. Ukweli unabakia palepale kuwa hakuna nadharia inayojitosheleza.

Nadharia ya Utu wa mwanadamu na Fasihi inathibitisha kuwa binadamu ndiye asili ya Fasihi, na Fasihi imebuni ufutuhi, utunzi ambao ndio msingi wa kazi hii. Nadharia ya fasihi na jamii inaamini kuwa kazi ya fasihi ni kuhifadhi historia ya jamii. Kwa kusoma kazi za fasihi tunaweza kupata historia ya jamii. Nadharia chimbuko la Fasihi inatambua kuwa mwanadamu ndiye mwanzilishi wa fasihi. Inasema fasihi ni sanaa inayotawala shughuli mbalimbali za jamii kama vile ibada, sherehe, mila na desturi, na nyinginezo. Kwa jumla kazi hii inaongonzwa na nadharia hizi tatu. Japo nadharia zote zinategemeana.

Kama mtafiti nimeona nadharia hii kama nguzo ya Dhima ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert kwaani mtunzi huyu ndiye haswa kiongozi aliye guswa na Nadharia Kiongozi.

SURA YA TATU

3.0 KAZI TANGULIZI

3.1 Utangilizi

Katika sura hii ya kazi tangulizi zinazo husu dhima ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert, mtafiti amejaribu kuzama kwa undani kuzichambua Riwaya nne za Shaaban Robert ambazo ni vitabu vya Kusadikika, Kufikirika, Siku ya watenzi wote na Adili na Nduguze. Lengo ni kutathimini kazi hizo na kuangalia mapengo au mapungufu yaliyoachwa na Tafiti katika tungo na maisha ya kila siku ya kijamii.

Sura hii inawasilishwa na machapishi mbalimbali yanayohusiana na mada hii ya utafiti. Machapishi haya yamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni uhakiki wa maandishi ya Shaaban Robert na yale ya asili yanayozungumzia ufutuhi katika kazi za Shaaban Robert. Kama Mtafiti nimezama kwa undani katika kuchambua Riwaya nne za Shaaban Robert ili kubaini matumizi mbalimbali ya ufutuhi katika kazi zake za uandishi.

Riwaya za Shaaban Robert zina mvuto wa pekee kwani zimefikirisha, ni fiche na hata msomaji akifika mwisho wa Riwaya bado anabakia na maswali akijiuliza mtafiti anayo shauku ya kuamsha ari kwa wasomaji na watunzi wa vitabu kufuata mfumo wa uandishi wa Shaaban Robert ambao una Mtiririko ulio bora umesheheni msamiati na misemo iliyokidhi mahitaji na vionyo vya jamii husika.

Azma kubwa ya mtafiti ni kuangalia mapengo au mapungufu yaliyoachwa na tafiti zilizotangulia kuhusiana na Dhima ya ufutuhi hususani katika Riwaya za Shaaban Robert mtafiti anahamasisha wasomaji na wakuza mitalaa kumuenzi Shaaban Robert na kutangaza kazi zake.

3.2 Tahakiki za Kazi Tangulizi

Kumekuwapo na kazi tangulizi katika kupanua wigo wa Lugha ya Kiswahili na kumuenzi Shaaban Robert. Tahakiki hizi mfano riwaya ya Ngoswe pendi kitovu cha uzembe, Morani na Prof. Emmanuel Mbogo, Watoto wa MamaNtilie na Prof. Emmanuel Mbogo, Giza limeingia na Prof. Emmanuel Mbogo, Tone la Mwisho zimeshughulika na Fani mbalimbali lakini fani ya Fasihi ya Lugha katika kipengele cha Ufutuhi kimefanyiwa kazi kidogo sana kwani ni fani inayofikirisha na inahitaji muda pamoja na vitendea kazi mbalimbali ili kufikia malengo yaliokusudiwa.

Riwaya nne za Shaaban Robert zilizoteuliwa na mtafiti zimeshughulika na harakati za kukuza maadili ndani ya jamii na kukuza vipaji vya waandishi na watunzi wa Kiswahili. Kazi tangulizi na machapishi ya Shaaban Robert na Riwaya zake baadhi ni kama hizi;

(1952), Adili na Nduguze; Macmillan, London,

(1951), Kusadikika, Nelson Nairobi

(1949), Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini, Nelson, Nairobi

(1954), Kielelezo cha Insha; Witwatersand, Nairobi

(1997), Methali na Mifano ya Kiswahili, TUKI, Dar es salaam

(1968), Kufikirika, Oxford, Nairobi

(1968), Utu bora Mkulima, Nelson, Nairobi

(1968), Siku ya Watenzi Wote, Nelson, Nairobi

(1967), Wasifu wa Siti bint Saad, Nelson, Nairobi

Mfano katika kufikirika ukurasa wa 37 Shaaban Robert anasema.

Kweli kama hebasi

Uongo nao matusi

Tena kweli almasi

Kitu azizi halisi

Uongo pia najisi

Mtu mwema haugusi

Tarijama “msema kweli mpenzi wa Mungu na anayo heshima ya pekee ndani ya jamii na maisha ya uongo ni mafupi na watu wanao uongo kama lebasu ghafla hujiona hawana nguo mbele ya wenzao”. Mfano wa Dhima ya ufutuhi katika Riwaya ya Siku ya Watenzi wote ukurasa wa (ix) ni ule mwanzo wa hadithi usemao.

Msimlizi: Paukwa

Msimliwa: Pakawa

Wote

Kaondoka Chanjagaa

Kajenga mji kakaa

Na mwanangu mwansiti,

Vijino kama yakuti,

Kinywani kama ukuta

Na viango vya kupita,

Tarijana - Maneno haya humwandaa msimuliwa kujiandaa kupokea masimlizi na kumfanya ahusike na kuvaa uhusika katika simulizi za kifutuhi kama hizo msimuliwa huvaa uhusika wa tatizo lakini mwishowe inaamsha ari ya kusoma, kutafiti na kuibuka na majibu mengi ya kisa mkasa kinachosimuliwa. Katika Riwaya ya Kusadikika ya Shaaban Robert ukurasa wa vii mtunzi anasema, “Ng’ombe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa

Tarijana: “mtu hakosi asili yake na kila mchumia juani hulia kivulini”. Ng’ombe ni kiashirio au kielelezo cha mtu anavyoweza kupata shida kubwa lakini msaada mkubwa hupata kutoka kwa Nduguze au kwao.

SURA YA NNE

4.0 MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

4.1 Usuli wa Kuingia Masikanini

Kwanza kwa kutumia barua rasmi ya ruhusa niliyopewa kutoka Chuo Kikuu huria cha Tanzania tawi la Dodoma. Kibali kutoka Mkurugenzi Mtendaji Halimashauri ya Wilaya ya Chamwino Kuanzia Juni 2011. Ziara ni mbinu iliyotumika kuingia Masikanini. Tafsiri ya ziara ni tendo la mtu kwenda eneo alilolenga na kukutana na wenyeji wake, kutembelea au kuzuru maeneo maalumu yaliyo kusudiwa kufanya mahojiano, kupiga picha, kuchukua vielelezo, video, kunasa sauti na kunukuu mambo muhimu yahasuyo ziara hiyo.

Hayo yote hutanguliwa na kupeleka taarifa katika eneo la ziara, kukutana na uongozi husika, kutambulishwa na kupewa maelezo muhimu kabla ya kuingia masikanini. Mtafiti alifika katika ofisi za chuo kikuu huria cha Tanzania Tanga na kujitambulisha tarehe 10/11/2011 halafu akaenda katika nyumba ya makumbusho Tanga mjini kujitambulisha na kupewa Dondoo za Shaaban Robert. Mkurugenzi wa makumbusho kuambatana na mtafiti hadi Machui Vibambani aliko zikwa marehemu Shaaban Robert.

Kijijini Machui/Vibambani mtafiti alipokelewa na uongozi wa mtaa na kutambulishwa kwa viongozi wa kijiji cha machui na kuruhusiwa kusaini vitabu vya mtaa wa kijiji tarehe 12/11/2011. Mtafiti alipelekwa moja kwa moja katika nyumba ya makumbusho ya marehemu Shaaban Robert akiwa pamoja na ndugu jamaa na majirani wa Shaaban Robert. Angalia picha vielelezo katika kurasa za 51 hadi 59 na 61 hadi 68.

Nilifanya mahojiano na ndugu hao ambao walieleza Nasaba zao na Shaaban Robert kazi alizofanya za kuunganisha koo, ujenzi na kutunga vitabu mbalimbali. Ndugu alipewa dhamana ya kutunza kaburi la Shaaban Robert Bwana Zongo yeye alifafanua kuwa Eneo la kaburi lile limekuwa kivutio na ni eneo la utalii kwani wageni wa ndani na nje ya nchi huzuru kaburi hilo. Makabila yaliyoko pale ni Wadigo, na Wasambaa Shughuli kubwa ya wakazi wa Machui ni uvuvi, biashara na kilimo, Pia kuna Machimbo ya chumvi inayopatikana ufukweni mwa bahari ya Hindi, wanawake hujishughulisha na ususi pamoja, biashara ndogondogo, kilimo na ufumaji.

4.2 Mbinu za Kukusanya Data

4.2.1 Dhana ya Mbinu Za Kukusanya Data

Mbinu za utafiti hutofautiana kutegemea na aina ya mada iliyolengwa, mazingira, lengo, mahitaji hali ya hewa, uwezo wa mtafiti kifikra kifedha, mila na desturi za watafitiwa na malengo makuu ya utafiti yanakuwa ndiyo kiini chake. Hivyo wanafalsafa wengi kama (Billey 1994) na (Sevenya na Robson 2001). Wanatoa fasihi ya Dhana ya mbinu za utafiti na kukusanya Data.

Kwa ujumla mbinu za utafiti usaili hatua za kifalsafa za mtafiti ambazo huzitumia kutafiti kukusanya data na kuandika taarifa. Data zinazotolewa ni matokeo ya utafiti husika, Baadhi ya mbinu za kukusanya Data ni usaili umakinifu, maswali na majibu, hojaji, ziara, vitabu na machapishi. Data nilizokusanya kutoka kwa watafitiwa huitwa data za msingi Data nyingine zinatokana na machapishi, vitabu na media.

4.2.2 Umakinifu

Ni mbinu muhimu ya utafiti ambapo mtafiti hujumuika na watafitiwa. Mfano mtafiti aliungana na ndugu wa marehemu Shaaban Robert kule Machui na kupata Historia yake kazi zake, wasifu wake na kuona jumba la makumbusho linalohifadhi kazi za Shaaban Robert. Pia mtafiti alitembelea kaburi la Shaaban Robert na kushiriki kufanya usafi wa mazingira pamoja na ndugu hao wakiongozwa na mjuukuu wa marehem Bi Asha Shaaban.

4.2.3 Usaili

Hii ni mbinu muhimu ambapo mtafiti hukutana na watafitiwa na kuongea nao kwa kuhojiana. (Seidman, 1991). Mfano nilikutana na baadhi ya wenyeji wasiofahamu Kiswahili lakini kwa vile viongozi wa kijiji walikuwepo walitumiwa kama wakalimani. Mila na desturi zilikuwa kikwazo kwani baadhi ya maeneo wanawake hawaruhusiwi kukaa mezani na wanaume kuongea au kujadiliana. Faida kubwa ya mbinu hii ilinisaidia kuonana ana kwa ana na watafitiwa.

4.2.4 Hojaji

Kwa kutumia mbinu hii niliandaa maswali yaliyoandikwa/chapwa yanayohusu mada iliyoteuliwa na kuwapatia watafitiwa husika kulingana na maelekezo ya jinsi ya kujaza, mbinu hii hutoa matokeo mazuri pale ambapo watafitiwa wenajua kusoma na kuandika. Niligawa Hojaji 320 kwa bahati nzuri walengwa wote walikuwa wanajua kusoma na kuandika ingawa ililazimu kufafanua maswali kwa badhi ya watafitiwa.

4.2.5 Wasaidizi Katika Kukusanya Data

Maeneo niliyoyateua yalihatiji kuwa na wasaidizi hasa kutokana na kutokuwa mwenyeji wa maneno hayo. Nilipata wasaidizi ambao walifanikisha zoezi la

kukusanya Data. Mfano kituo cha makumbusho Tanga, Vibambani na Machui Tanga, Kigamboni Dar es Salaam na Mpwapwa Chuo cha utafiti wa mifugo.

4.3 Zana za Utafiti

Zana za utafiti ni vitendea kazi ambavyo nilivitumia kufanikisha utafiti, nilitumia kalamu, Daftari, karatasi, manila kamera (picha) zake vitatumika kwenye matukio ya moja kwa moja.

11. RATIBA

Jedwali Na 4.1: Kuonesha Ratiba ya Kazi ya Utafiti

MWAKA	SHUGHULI	J	F	M	A	M	J	J	A	S	O	N	D
2011	Kuandaa Pendekezo la utafiti												
2011	Kuwasilisha pendekezo la utafiti												
2011	Kukusanya Data kwa Kina												
2011	Kuchambua Data												
2011	Kuandaa Tasnifu ya awali ya Utafiti												
2012	Kuwasilisha Tasnifu Sahihisho ya II												
2012	Kurekebisha Masahihisho ya II												
2012	Kufanya Masahihisho ya Mwisho												
2012	Kuwasilisha Tasnifu ya Mwisho												
2012	Utahini												

Chanzo: Mtafiti

4.5 Bajeti

Bajeti ni mpango mzima unaoonesha mwelekeo wa mapato na matumizi hivyo kutoa dira ya kazi mzima kulingana na mapato yanayotarajiwa. Vyanzo vya mapato tarajiwa ndio mwongozo wa mpango mzima. Gharama zote za utafiti zilifikia Tsh. 8,500,000/=.

Bajeti hii inaonesha vyanzo vya mapato na matumizi kama ifuatavyo:

Jedwali Na 4.2: Kuonesha Bajeti ya Kazi ya Utafiti

VYANZO VYA MAPATO				
Mhusika/Mchangiaji	Tsh	Shughuli	Kiwango (Tsh)	Jumla (Tsh)
Vyanzo binafsi	1,100,000	Karatasi (Rimu)	4@10000/=	40000/=
Mashirika yasiyo ya Serikali	1,000,000/=	Kucharaza kwa ngamizi	Kurasa 50@1,000/=	500,000/=
Wahisani	5,700,000/=	Karudufu	Kurasa 400@50/=	200,000/=
Watu/Jamii	700,000/=	Kalamu	40@250/=	10,000/=
		Video kamera	1@1.200,000/=	1,200,000/=
		Vifaa vya ziada		800,000/=
		Laptop	1@800,000/=	800,000/=
		Printa	1@400,000/=	400,000/=
		Uhariri	Kurasa500@3000/=	1,500,000/=
		Usafiri (Nauli)	Siku 50@10000/=	500,000/=
		Posho ya kujikimu	Kujikimu siku 60@20,000	1,200,000/=
		Wasaidizi	4@10000/=	400,000/=
		Kuandaa ripoti		200,000/=
Jumla	8,500,000			8,500,000/=

Chanzo: Mtafiti

SURA YA TANO

5.0 UCHAMBUZI WA DATA

5.1 Utangulizi

Uchambuzi wa data hujumuisha upatikanaji wa data mbalimbali zikiwemo data za msingi data za upili na za asilia hivyo zoezi la kuzichambua linaambatana na ukamilishwaji wa kazi ya mtafiti kwa kuwezesha na watafitijwa na mbinu nyinginezo za mawasiliano.

5.2 Madhumuni ya Kiini cha Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa Data hufanyika pale ambapo mtafiti amekamilisha upatikanaji wake. Hivyo Data ndiyo kiini cha kazi ya mtafiti, kupitiya uchambuzi huu takwimu halisi hutolewa kama zao la kazi nzima ya mtafiti. Hili ni zoezi la kujumuisha matokeo ya utafiti mzima. Hivyo tunaweza kusema uchambuzi wa Data ndicho kiini cha kazi nzima ya utafiti pia ni dira ya matokeo yote ya kazi iliyolengwa.

Idadi ya wateuliwa katika uteuzi huu umezingatia maeneo ya kufanyia kazi hii. Maeneo hayo ni Dodoma mjini, Mpwapwa, Tanga mjini na Vijiji vya Machui/Vibambani na Dar es Salaam Kigamboni waliko baadhi ya ndugu na jamaa wa Shaaban Robert. Hivyo jumla ya wahojiwa ni 320.

5.3 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa Data na uwasilishaji wake umefanyika kwa makini sana sababu maswali yaliyotumika kwenye mahojiano yalilenga kujua kazi za Shaaban Robert na kwa kuwa waliohusika katika mahojiano ni wa rika mbalimbali, Hivyo hata majibu yalitofautiana, Mfano

Swali la kwanza:

“Je, kuna matukio gani ya kifutuhi yanayojitokeza kwenye Riwaya za Shaaban Robert na je yana Dhana yoyote?”

Baadhi ya wahojiwa walitoa majibu mafupi. Mfano

- (ii) Ndiyo
- (iii) Yana Dhana ya kutoa maonyo
- (iv) Shaaban Robert alikuwa mwalimu wa Lugha.

Majibu yalitofautiana kutegemea na upeo wa Elimu aliokuwa nayo mhojiwa. Mfano wanafunzi wanasoma somo la Kiswahili waliweza kuchambua zaidi Riwaya za Shaaaban Robert na Dhima mbalimbali ya ufutuhi kwa kulinganisha vitabu vyake walivyosoma. Data na majibu zimeandikwa na kuoneshwa kwa kuanishwa kwenye majedwali kwa kuonesha idadi ya wahojiwa na washiriki na asilimia zao.

5.4 Aina ya Data

Data inayotumika katika kazi hii inatokana na Mkusanyiko wa taarifa na majibu mbalimbali ya maswali kadhaa, yaliyoulizwa toka kwa watoa taarifa maskanini na zile ambazo zimetoka kwenye kazi zilizo tangulia.

5.4.1 Data za Msingi

Chimbuko la upatikanaji wa data hizi ni kwenye eneo la utafiti ambalo mtafiti anakwenda mwenyewe na kuzipata Data hizi kwa kuzikusanya kutumia zana mbalimbali.

5.4.2 Data za Upili

Data za Upili ni zile zinazotokana na machapishi kama vile vitabu, wavupepe na majaridha. Mtafiti huweza kuzipata Data hizi kwa njia ya usomaji wa vitabu, usomaji

wa machapishi na wavupepe, Hivyo mtafiti amazikuta Data hizi ziko tayari hivyo yeye huzichambua na kuchukua zile zenye maudhui yanayolenga kazi yake aliyoiandaa.

5.5 Uwasilishaji wa Data

Data zinazowasilishwa hususani katika kazi hii ya utafiti, umezingatia matokeo ya taarifa ya data zilizopatikana hasa baada ya uchambuzi. Kila jibu la swali la udadisi linatakiwa kuwasilishwa likiwa limejitegemea kwa kutumia njia mbalimbali mfano Michoro, maelezo au jedwali.

Lengo la kuteua njia ya uwasilishaji wa Data ni kutegemea na watafitiwa wanavyoweza kutoa majibu kutokana na uelewa wao, umri, Elimu, Mila na Desturi, mawasiliano au lugha na mazoezi. Chimbuko la Data iliyopo katika utafiti huu imetokana na jitihada nilizofanya kukusanya taarifa mbalimbali.

Jedwali Na. 5.1: Kuonesha Takwimu za Majibu ya Watafitiwa

Sn	Aina Ya Ufutuhi Ulioainishwa	Idadi Ya Washiriki	Waliosema Wanajua	Waliosema Hawamjui	%	Waliosema Hawana Uhakika	%
01	Katika Nyimbo	320	180	110	90.6	30	9.4
02	Hadithi	320	150	140	90.6	30	9.4
03	Tungo	320	90	50	43.75	180	56.25
04	Katika Mashairi	320	300	4	95	16	5
05	Katika Riwaya	320	210	30	75	80	25

Chanzo: Mtafiti

Jedwali Na. 5.2: Maswali ya Utafiti

Swali: Je matukio haya ya ufutuhi yana Dhana yoyote?

Sn	Dhana Zilizotajwa	Idadi Ya Washiriki	Waliosema ni Kweli	%	Waliosema Si Kweli	%	Waliosema Hawajui
01	Kufundisha Jamii	320	300	93.7	1	0.31	19
02	Kufurahisha	320	320	100	0	0	0
03	Kuongeza Matumizi ya Kejeli Ubeuzi, Vijembe na Dhihaki	320	50	15.6	250	78.13	30
04	Kuibua Ari ya Usomaji na Uandishi	320	300	93.7	5	0.56	15
05	Kuibua Moyo wa Utafiti	320	295	92.9	5	0.56	20
06	Kueneza Dini ya Kiisilamu	320	50	15.6	100	31.25	70
07	Kukuza Lugha ya Kiswahili	320	310	97	5	0.56	5
08	Kutangaza Familia ya Shaaban Robert	320	5	1.56	300	93.7	15
09	Kupiga Vita Ukoloni na Unyanyasaji	320	300	93.7	5	0.56	15
10	Kuimarisha Familia, Undugu, Malezi Namakuzi Bora Katika Familia	320	312	97.5	3	0.93	5

Chanzo:**SWALI 2 na jinsi lilivyo jibiwa na watafitiwa****SWALI**

Ni katika Muktadha/miktadha gani Shaaban Robert ametumia matukio ya kifutuhi katika Riwaya zake?

Swali hili lilijibiwa kwa na watafitiwa wengi na kutoa maelezo kutokana na jinsi kila mmoja anavyo mfahamu Shaaban Robert.

- (ii) Wapo walomsimulia Shaaban Robert kwa umahiri wake katika uandishi wa vitabu.
- (iii) Umahili wa Shaaban Robert katika mashairi zaida ya asilimia sabini walikiri kuwa mwandishi huyu hana mpinzani.
- (iv) Dhima kubwa ya ufutuhi katika Riwaya zake walitaja mfano kusadikika kufikiria, Adili na Nduguze, Maisha yangu na baada ya miaka 50. Kuwa ni vitabu ambavyo havijapoteza umaarufu kwa stadi zilizomo ndani yake vinatoa mafunzo kwa rika zote na mazingira mbalimbali.
- (v) Watafitiwa wanamchora Shaabani Robert na kumuona kuwa ni kioo cha lugha ya Kiswahili. Wanatoa wito kwa serikali kumuenzi Gwiji huylu kwa Kiswahili kwa kuingiza vitabu vyake vyote kwenye mtalaa wa somo hili ambalo ndiyo lugha ya taifa.
- (vi) Ubunilizi, lugha fiche na msamiati aliotumiya Shaabani Robert katika Riwaya mbili za Kusadikika na Kufikirika zilizosomwa na watu wengi, majibu yalio tolewa na watafitiwa wote 320 yameonesha mvuto, ushawishi, na kuamsha ari ya usomaji wa vitabu. Aidha wameshauri taasisi mbalimbali kuendelea kuchapisha na kusambaza vitabu ivyo katika shule na maktaba zote nchini.

SWALI 3.

Je, ni athari gani zinazoweza kusababishwa na dhima ya ufutuhi katika Riwaya za **Shaaban Robert?**

Jedwali Na. 5.3: Kuonesha Majibu ya Watafiti wa Juu ya Swali Na.3 (Athari za Dhima ya Ufutuhi)

SN	Athari Zilizoinishwa	Idadi ya Washiriki	Waliosem a Kweli	%	Waliosem a si Kweli	%	Waliose ma Hawaju i	%
01	Kuamsha Ari ya Kusoma Vitabu Kwa Bidii Zaidi	320	300	93.7	10	3.12	10	3.12
02	Kuongeza Uwezo wa Kutafiti Lugha ya Kiswahili Na Misamiati	320	200	62.5	50	15.6	70	21.87
03	Ka Toa Elimu Juu ya Kanuni Za Kutunga Vitabu	320	310	96.87	5	1.56	5	1.56
04	Kuibua Moyo wa Ubunifu na Matumizi Bora ya Maneno ya Kiswahili	320	320	100	0	0	0	0
05	Kukatisha Tamaa Watunzi na Waandishi Wachanga(Lugha Ngumu)	320	20	6.25	200	62.5	100	31.25
06	Ubunilizi Unaotumika Kutoendana na Hali Halisi ya Kizazi Kilichopo.Kupoteza Maana/Mvuto	320	50	15.6	250	78.12	20	6.25
07	Kuhamasisha Wakuza Mtaala Kutoa Maelekezo ya Ufundishaji wa Somo La Kiswahili	320	300	93.75	2	0.63	18	5.63
08	Kuelimisha Walimu wa Kiswahili Kutumia Mbinu Bora za Kufundishia Somo Hilo	320	150	48.9	50	15.6	120	37.5
09	Kuimarisha Juhudi za Kumuenzi Shaaban Robert na Kazi Zake za Uandishi wa Kiswahili	320	300	93.75	0	0	20	6.25

Chanzo: Mtafiti

SURA YA SITA

6.0 MHUTASARI NA MAPENDEKEZO

6.1 Muhtasari

Utafiti umechunguza mchango mkubwa wa Shaaban Robert katika kukuza Dhima ya ufutuhi katika kazi zake. Utafiti umehusisha watu wa rika mbalimbali wkiwemo wake kwa waume. Asilimia 31 walikuwa ni vijana hususani walioko shuleni (Sekondari), vyuo vya Elimu ya juu Asilimia 40.62. Asilimia 12.5 walikuwa ni watumishi kama walimu, kada nyingine serikalini na mashirika mbalimbali. Asilimia 9.4 walikuwa ni wananchi wa kawaida na Asilimia 6.25 viongozi wa dini na Taasisi mbalimbali, waasisi wa lugha ya Kiswahili na magwiji wa Lugha hii.

Matokeo ya kazi hii ya utafiti yameonesha kuwa kundi kubwa la vijana hawamfahamu sana Shaaban Robert kutokana na vitabu vyake kutochapishwa kwa kipindi takriban miaka kumi iliyopita kuanzia miaka ya 1990. Hivyo vitabu vyake havikuwepo kwenye muhtasari wa Kiswahili badala yake walisoma Riwaya nyingine.

Lakini inaonekana kuwa walimu wa Kiswahili zaidi ya asilimia 80% walitumia vitabu vya Shaaban Robert kama marejeleo katika somo hili, hivyo kuwafanya wasomaji kumfahamu mtunzi huyu kwa undani zaidi. Kutokana na vitabu vya Shaaban Robert kuwa na mvuto mkubwa walimu wa Kiswahili hususani vyuo vya elimu ya juu hawakusita kumtambua kama Gwiji la Kiswahili. Hadi sasa riwaya za Shaaban Robert ndizo kitovu cha somo hili katika vyuo hivi.

Utafiti umeonesha kuwa wachapishaji wa vitabu na hususan nyota na mkuki wanastahili kupewa sifa na tuzo kuu kwani wanachapisha vitabu vyote vya Shaaban Robert vilivyopotea mfano riwaya za Siku ya watenzi wote, Adili na Nduguze, Kufikirika na Kusadikika na kujitahidi kuvisambaza katika taasisi za Serikali na watu binafsi.

Kundi la watu wazima hata wale wasiojua kusoma na kuandika kwa kupita masimulizi wameonesha kumfahamu na kumtambua Shaaban Robert. Hii inadhihirisha kuwa Shaaban Robert alikuwa na uwezo mkubwa kwa kuishi na jamii yoyote ile na alitambua umuhimu uwezo wa kila mwanajamii, tabia pamoja na mchango wake kifikra na alithamini sana mahusiano bora ndani ya koo na jamii za kiafrika. Katika kutimiza azma hii Shaaban Robert alithamini fasihi simulizi hivyo wasiojua kusoma walielewa kazi zake Mfano halisi wakazi watu wazima katika vijiji vya Pangani Machui na Vibambani Tanga hawa wanaelewa zaidi kazi za Shaaban Robert kupitia fasihi simulizi na wanaendelea kuzirithisha kwa kizazi kilichopo kwa masimulizi.

Kazi hii ilijitoma katika kuangalia matumizi ya ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert. Na uchambuzi wa kina ulifanywa kwa kuzingatia Riwaya nne ambazo ni kusadikika, kufikirika, Adili na nduguze, siku ya watenzi wote. Riwaya hizi zimeonesha uwezo mkubwa wa Shaaban Robert katika Lugha fiche, kuzuia ubeuzi kutumia msamiati unaolenga kumfikirisha msomaji kufurahisha na kumfanya msomaji kuvaa sura ya mtendewa au (mtendaji husika).

Wengi wa watafitiwa wanasema kuwa kazi za Shaaban Robert zinahitaji kutangazwa zaidi na pengo limeonekana miongoni mwao. Hususan wale wanaosoma sekondari

huwatambua zaidi waandishi wa vitabu vya Kiswahili walio bado hai huku wakisahau hazina kubwa na shehena ya utaalumu wa uandishi kutoka kwa marehemu Shaaban Robert.

Aidha linajitokeza tatizo kubwa la upungufu wa vitabu vya Kiswahili katika maktaba za shule na vyuo. Mfano asilimia 60% ya shule taasisi na vyuo alivyotembelea mtafiti zilikuwa na upungufu mkubwa vitabu ambapo uwiano ni 1:15 hadi 20. Kila jamii inao utaratibu wa kutunza Historia ya mila na desturi zao, Mtafiti alihamasika kuona linajengwa jengo la makumbusho ya kazi za Shaaban Robert kijijini Machui. Pia limejengwa imara ingawa wanafamilia wengine ambao wamezikwa pale mfano bintiye Mwanjaa Kaburi zao hazijatengenezwa.

Namshukuru sana Mkurugenzi wa makumbusho ya Taifa Tanga kutambua mchango wa Shaaban Robert katika kukuza Lugha ya Kiswahili kwa kutenga chumba/eneo maalum kwa kazi zake na machapishi mbalimbali. Aidha kituo kimetayarisha waongozaji mahiri wanaomjua na kufahamu kazi za shaaban Robert ambao mara zote huongoza wageni, watalii na makundi maalum yanayohitaji kuzuru kaburi la Shaaban Robert na kupata Historia ya maisha yake na kazi zake kwa ujumla.

6.2 Mapendekezo

Katika sehemu hii nilipata maoni na mapendekezo kutoka makundi yote niliyotembelea na kufanya mahojiano. Mapendekezo mengi yanafanana hivyo yameunganishwa na kutolewa kulingana na makundi husika. Wachapishaji wa vitabu vya Kiswahili wachapishe vitabu vingi vya Shaaban Robert vinavyokidhi mahitaji shuleni na vyuoni.

Ufutuhi ni njia rahisi ya kufundishia na kufikisha ujumbe ivyo jamii ihamasishwe kutumia njia hii na kuruhusu tafiti zaidi juu ya ufutuhi kufanyika. Walimu wa Lugha ya Kiswahili wapewe mafunzo kila wakati ili wawe mabingwa wa somo hilo na kuongeza uwezo wa kuchambua vitabu vya Kiswahili na mbinu bora za ufutuhi katika utunzi wa vitabu.

Waalimu wahamasishe wanafunzi kusoma vitabu kutunga na kusimamia kazi zao za kisanii kwa kutangaza mashindano na kutoa tuzo kwa kufuata misingi ya Shaaban Robert. Wizara ya Elimu iweke vitabu vya Shaaban Robert katika mtalaa ili kuhimiza ufundishaji, uzalendo na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

Viongozi waelekezwe kuyaenzi na kuhifadhi maeneo ya kihistoria aliyofanyia kazi Shaaban Robert mfano Sekondary ya old Tanga, Mpwapwa chuo cha mifugo, misikiti aliyosali kama Mpwapwa, miti aliyopanda mfano minazi vitalu vilivyoko Mpwapwa, kuhifadhi vyanzo vya maji ambavyo vilimhamasisha hadi kutunga mashairi mfano kijito chenye njia panda mbili kilichopo Mpwapwa, choo na chumba alichoiishi kule Mpwapwa chuo cha mifugo.

Jamii ihamasishwe kuzipenda, kuzienzi na kuzitangaza mila na desturi njema alizotufundisha shaaban Robert na kutumia ufutuhi wa hali ya juu katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa walengwa kwani Ufutuhi unaongeza ari ya kusoma na kujifunza kwa kuifanya kazi ya mwanazuoni husika iwe na thamani kubwa. Elimu zaidi itolewe kwa watanzania ili waitambue lugha ya Kiswahili kuwa ni lugha yao ya Taifa hivyo wajivunie kutumia Kiswahili wakati wote.

Watafiti wanaochukua Shaaban Robert kama sehemu ya utafiti wao waeleze jamii, kupitia vyombo mbalimbali vya mawasiliano kutangaza kazi za Shaaban Robert hasa kipengele cha ufutuhi. Vikundi vya komedi vilivyoanzishwa viimarishwe ili kuimiza ufundishaji kwa njia ya ufutuhi

MAREJELEO

- Bailey , K. D. (1994), *Methods of Social Reaserch*, Chikango Maxwell Maemillan International.
- Denscombo, M, (2005), *The Good Reaserch Guide for Small Scale Social Reaserch Projects*, New York,Open University Press.
- Egleton T, (1996), *Literary theory: An Introduction (2nd Edt)*, MASSACHUSETTS Blackwell Publishing.
- Edwin Semzaba (1988) *Ngoswe Penzi kitovu cha uzembe*
- Gibbe, A. G. (1978), *Shaaban Robert: Mshairi Dar es Salaam, Taasisi ya Chunguzi wa Kiswahili*
- Gibbe, A. G. (1990), *Ufumbaji katika Ushairi wa Kiswahili katika Kiswahili Juz. Ya Gibbe A., G. (mhariri) Mhariri Education).*
- Geihard, E, (1964), “The New Hermeneutics and the Early Luther” *Theology today* Juzuu ya 21. , katika.
- [http:// en wikipedia. Org/ wiki/Hermeneutics](http://en.wikipedia.org/wiki/Hermeneutics) iliyosomwa tarehe 24/12/2008
- Kezilahabi, E, (1976), *Shaabani Robert Mwandishi wa riwawaya” (Haijachapishwa) Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*
- Kimaro Z, K, (2008). *Shaaban Robert mtetezi wa Wanawake “(haijachapishwa) Ripoti yaUtafiti Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*
- Massamba D, P,B, (2004), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha Dar es Salaam Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*
- Momanyi,C, (2001), *Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert, katika Kiswahili Juz 64 Y.M. Kihore (mhariri) Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.*

- Msokile , M, (1992), Misingi ya Hadirth Fupi Dar es Salaam, Dar es Salaam University press.
- Mulokozi, M, M Na Kahigi, K, K, (1979), Kunga za Ushairi na Diwani yetu. Dar es Salaam. Tanzania Pubshing House.
- Ndulute, C,(1994), The poerty of Shaaban Robert, Dar es salaam. Dar es Salaam. Dar es Salaam Universitr Press.
- Newton,C, (1994), Twentieth century Literry Theory (2nd Edt), New York,St. Martins Press.
- Robert, S, (1951), Kusadikika, Nairob i, Nelson.
- Robert, S, (1952) , Adili na Nduguze, London, MaCmillan.
- Robert, S, (1968), Kufikirika, Nairobi, Oxford.
- Robert, S, (1968), Siku za Watenzi Wote, Nairobi, Nelson.Sengo, T.S
- Na Kiango, S.D,(1973), Hisi Zetu, Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Kiswahili.
- Sengo, T.S, (1975), Shaaban Robert: Uhakiki wa maandishi yake. Nairobi, Kenya Litho limited.
- Sengo, T.S.Y, (2009), Fasihi za Kinchi, Dar es Salaam, AERA Kiswahili Researcher Production.
- Senkoro,F.E.M.K, (1987), Fasihi na Jamii, Dar es Salaam, Press and Publicity Centre.
- Seidman, I,E, (1991), Interviewing & Qualitative Reserch A Guide for Reaserch.In Education and Social Science, New York, Teachers College Press.
- SevenyeW.C. and Robinson, R.M, (2001), Qualitative Reaserch Isues and Methods, AIntroducton for Education Technologists, USSA Arisona.

- Ponella Athuman (2007) – Tasnifu ya M.A Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma
Maktaba ya Chuo Kikuu Dodoma.
- Wafula, R.M, (2007), Nadharia za Uhakiki wa Fasihi, NAIROBI, Sai Industries
Limited.
- Wamatila, K.W, (2002), Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele vyake, Nairobi,
Phoeni Publishers Limited.
- Bailey,K.D, (1994), Method of Social Reaserch, Chikago, Maxwell Macmillan
International.
- Coombes, H, (1959), Literature and Criticim, Kanberra, Catto and Windus.
- Econ, C.J, (1995), Education, Reaserch, Statistics and Measurement, Kampala,
Makerere University.
- Kihore, Y.M, (2002), Jaridala Uchaguzi wa Kiswahili, Juz.65, Dar es Salaam,Chuo
Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kipingu, P.R, (2009), M.A, TheatreArts, Dessertation, Dar es Salaam University of
Dar es Salaam.
- Mazibuko, L.C.J, (2007), Ph. D Thesis, Invetory of Malawi's Intangible Cultural
Heritage, Lilongwe, Malawi, (Unpublished).
- Msanjila, Y.P, (2003), Kushuka kwa Hadhi ya Lugha za Jamii nchini Tanzania, Dar
es Salaam, Tanzania Publishing House.
- Sevenye, W.C and Robinson, R, (2001), Qualitative Reaserch Issues and Methods,
An Introduction for Educational Technologists, USA, Arisona.
- Seidman, I, E, (1991), Interviewing & Qualitative Reserch. A Guide for Reaserch.
In Education and Social Science, New York, Teachers College Press.
- Tasisi ya Ukuzaji Mitalaa, (1989), Kiswahili Secondary, Dar es Salaam, Taasisi ya
Ukuzaji Mitaala.

- Warele and Warren,(1949), Theory of Literature, London, Penguin Books.
- Bailey, K. D, (1994), Methods of Social Reaserch, Chikago, Maxwell Macmillan International.
- Denscombo, M, (2005), The Good Reaserch Guide foa Small Scale Social Reaserch Projects, New York, Open University Press.
- Massamba, D, P, B, (2004), Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha, Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Seidman, I. E, (1991), Interviewing & Qualitative Reaserch. A Guide for Reaserch in Education and Social Science, New York, Teachers College Press.
- Sevenye, W. C. and Robinson, R, (2001), Qualitative Reaserch Issues and Methods, An Introduction for Educational Technologists, USA, Arisona.
- Sengo, T.S.Y, (2009), Fasihi za Kinchi, Dar es Salaam, AERA Kiswahili Researcher, Products.
- Geihard, E, (1964), “The New Hermeneutics and the Early Luther”, Theology today Juzuu ya 21.1, katika <http://en.wikipendia.org/wiki/Hermeutics> iliyosomwa tarehe 24/12/2008
- Eagleton, T, (1996), Literary theory: An Introduction (2nd Edt), MASSACHUSETTS, Blackwell Publishing.
- Gibbe, A.G, (1978), Shaaban Robert: Mshairi, Dar es Salaam, Taasisi ya Chunguzi wa Kiswahili.
- Gibbe, A. G, (1990), “Ufumbaji katika Ushairi wa Kiswahili katika Kiswahili, Juz. Ya 1, Gibbe,G (mhariri), Education.
- Kezilahabi, E, (1976), “Shaabani Robert Mwandishi wa riwaya” (Haijachapishwa), Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Kimaro, Z. K, (2008), “Shaaban Robert mtetezi wa Wanawake” (haijchapishwa),
Ripoti ya Utafiti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Lucas, F.L (1967) Tragedy Serious Drama in Relation to Aristotles Poetics London
- Momanyi, C, (2001), Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert,
katika Kiswahili, Juz. 64 Y.M. Kihore (mhariri). Dar es Salaam, Taassisi ya
Uchunguzi wa Kiswahili.
- Msokile, M, (1992), Misingi ya Hadithi Fupi, Dar es Salaam, Dar es Salaam
University Press.
- Mulokozi, M. M, na Kahigi, K. K, (1979), Kunga za Ushairi na Diwani Yetu. Dra es
Salaam, Tanzania Pubshing House.
- Ndulute, C, (1994), The Poetry of Shaaban Robert, Dar es Salaam. Dar es Salaam,
Dar es Salaam Universitr Press.
- Newton, C, (1994), Twentieth century Literary Theory (2rd Edt), New York, St.
Martins Press.
- Robert, S, (1951), Kusadikika, Nairobi, Nelson.
- Robert, S, (1952), Adili na Nduguze, London, MacCmillan.
- Robert, S, (1968), Kufikirika, Nairobi, Oxford.
- Robert, S, (1968), Siku za Watenzi Wote, Nairobi, Nelson.
- Richard Janko (1984) – Aristotle on comedy
- Salingar, L. shake speare
- Senkoro, F. E. M. K, (1987), Fasihi na Jamii, Dar es Salaam, Press and Publicity
Centre.
- Sengo, T. S na Kiango, S.D, (1973), Hisi Zetu, Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi
wa Kiswahili.

Sengo, T. S, (1975), Shaaban Robert: Uhakiki wa maandishi yake. Nairobi, Kenya

Ltd.

Prof. Emmanuel Mbogo (2009) – Watoto wa MamaNtilie

Prof. Emmanuel Mbogo (1991) – Giza limeingia

Prof. Emmanuel Mbogo (1996) – Tone la Mwisho

Prescott, H. W (1929) The comedy of errors.

USSber, RIG (1977) – Old comedy and character

MAREJELEO**B.SAMPULI YA MAREJELEO YA WASAILIWA WATAFITIWA****(WATAFITIWA 105 KATI YA 320)**

SN	Jina La Mtafitiwa	JINSI	Cheo / Wadhifa / Kazi
1	Mathew Ngowi	ME	Kiongozi Wa Taasisi
2	Moses Benedicto	ME	”
3	Edwin Kisango	ME	“
4	Daudi Pungwe	ME	“
5	Eduard Kandege	ME	“
6	Anamaria Kidunda	KE	“
7	Amina Mussa	KE	“
8	Rosemary Mpagama	KE	“
9	Julieth Pesambili	KE	“
10	Aisha Kimolo	KE	“
11	Shekh Abubar Ibrahim	ME	Kiongozi Wa Dini / Taasisi
12	Fr Daudi Ngimba	ME	“
13	S.R Margreth Chuma	KE	“
14	Caroline Kimwaga	KE	“
15	Fatuma Mwenda	KE	“
16	Mary Mathew	KE	“
17	Jane Nko	KE	“
18	Janerose Madoshi	KE	“
19	Elias Shenkalwa	ME	“
20	Juma Mazinge	ME	“
21	Amani Matonya	ME	Wanafunzi
22	Burtholomeo Mnyambwa	ME	“
23	Chidawili Sendwa	ME	“
24	Chihawa Fwalu	ME	“
25	Jacobo Mkankule	ME	“

26	Kafalu Nkwawa	ME	“
27	Mashaka Malewa	ME	“
28	Ramadhani Ngalya	ME	“
29	Rupami Lumanywa	“	“
30	Benjamini Peter	“	“
31	Emanuel John	“	“
32	Fedrick Charles	“	“
33	Gidion Isaka	“	“
34	Isaya Elisha	“	“
35	Jackson Pallingo	“	“
36	John Zakayo	“	“
37	Labani Patrick	“	“
38	Lazaro Mtumwa	“	“
39	Majuto Dotoni	“	“
40	Mtyani Mojelwa	“	“
41	Noel Nghusule	“	“
42	Stephano Maulya	“	“
43	Yohana Dede	“	“
44	Agnes Malogo	ME	“
45	Beatrice Maulya	“	“
56	Damarisi Masagari	“	“
57	Elizabeth Makomolo	“	“
58	Faustina Yohana	“	“
59	Janeth Madeha	“	“
60	Janeth Barua	“	“
61	Julia Mbishai	“	“
62	John Mlolwa	Me	Vyuo Vya Elimu Ya Juu
63	Amani Mwaluko	“	“
64	Amani Gresford	“	“
65	Amax Chibago	“	“

66	Emanuel Eliah	“	“
67	Gerishomu Mwaluko	“	“
68	Ibrahimu Nduhani	“	“
69	Isaka Madeha	“	“
70	John Ndilito	“	“
71	Joseph Kabia	“	“
72	Lkedmoni Mkwai	“	“
73	Lister Ndumila	“	“
74	Moses Mtemi	“	“
75	John Balisidia	“	“
76	Agnes Ndalul	Ke	“
77	Christina Daudi	“	“
78	Ester Mhando	“	“
79	Evelina Malogo	“	“
80	Ever Benjamini	“	“
81	Janeth Duka	“	“
82	Leah Mtyani	“	“
83	Mariam Duka	“	“
84	Mwasiti Mabefu	“	“
85	Neema Edward	“	“
86	Neema Makome	“	“
87	Pendo Machelmba	“	“
88	Pendo Edward	“	“
89	Neema Makome	“	“
90	Sechelela Twalale	“	“
91	Shukurani Mkwai	“	“
92	Sikujua Mpilimi	“	“
93	Tiriza Stanley	“	“
94	Zena Chibago	“	“
95	Eddina Madila	“	“

96	Agnes Magnus	“	“
97	Elizabeth Malogo	“	“
98	Lucy Misile	“	“
99	Pendo Stephano	“	“
100	Tabu Fundi	“	“
101	Pascal Malema	Me	Wasiowatumishi
102	Ramadhani Mwiga	“	“
103	Peter Pandisha	“	“
104	Anna Claudio	Ke	“
105	Rosemary Leornad	“	“

VIAMBATISHI

Picha Na.1



Kaburi la Marehemu Shaaban Robert Lililoko Machui – Vibambani Tanga
Mtafiti Pamoja na Mjukuu wa Marehemu Aitwaye Asha (Kulia)

Picha Na.2



Kijijini Machui Baada ya Kupokrlewa Ndugu na Jamaa wa Shaaban Robert



Picha Na.3: Mtoto wa Kiume wa Shaaban Robert Aitwaye Iqbal (Yuko Hai)



Picha Na.4: Jengo la Choo Alichotumia Shaaban Robert Mpwapwa



Picha Na.5: Ndugu Aneyehudumia Kaburi la Shaaban Robert Machui Kijijini

Aitwaye Zongo Aliyeketi na Mtafiti



Picha Na. 6: Mtafiti Alipofika Chuo Huria Cha Tanzania Tanga – Juni 2012



Picha Na.7: Katikati Makamu Mkuu wa Chuo Lit Mpwapwa Kushoto Mzee Mbeho
Aliyefanya Kazi na Shaaban Robert



Picha Na.8: Marehemu Shekh Alli Khamisi Liembe wa Mpwapwa Rafiki wa
Shaaban Robert Mwanzilishi wa Msikiti Mkuu – Mpwapwa



Picha Na. 9: Mtafiti Aliporipoti Katika Kituo Cha Makumbusho Tanga Mjini
Tarehe 9 Novemba 2011